# القرآن الحكيم

# QURANI TAKATIFU

Swahili Quran Translation

by
Sheikh Abdullah Saleh Al-Farsy
(Former Chief Kadhi of
Zanzibar & Kenya)

110. (Hawataamini); na tutazigeuza nyoyo zao na macho yao kama wasivyoamini mara ya kwanza; na tutawaacha katika maasiya yao wakitangatanga ovyo.

وَنُقَلِّبُ أَفْئِدَتَهُمْ وَأَبْصَارَهُمْ كَمَا لَمْ يُؤْمِنُوا بِهِۦٓ أَوَّلَ مَرَّةٍ وَنَذَرُهُمْ فِى طُغْيَٰنِهِمْ يَعْمَهُونَ ﴿١١٠﴾

111. Na lau kama tungewateremshia Malaika (kuwashuhudilia Ujumbe wa Nabii Muhammad kama walivyotaka), na wafu wakazungumza nao (kuwa haya ni kweli), na tukawakusanyia kila kitu mbele yao (kikawambia haya pia), wasingaliamini isipokuwa atake Mwenyezi Mungu (kuwatenza nguvu mpaka waamini). Lakini wengi wao wamo ujingani.

وَلَوْ أَنَّنَا نَزَّلْنَآ إِلَيْهِمُ ٱلْمَلَٰٓئِكَةَ وَكَلَّمَهُمُ ٱلْمَوْتَىٰ وَحَشَرْنَا عَلَيْهِمْ كُلَّ شَىْءٍ قُبُلًا مَّا كَانُوا لِيُؤْمِنُوٓا إِلَّآ أَن يَشَآءَ ٱللَّهُ وَلَٰكِنَّ أَكْثَرَهُمْ يَجْهَلُونَ ﴿١١١﴾

112. Na namna hii tumemfanyia kila Nabii maadui; (nao ni) mashetani katika watu na (mashetani katika) majini. Baadhi yao wanawafunulia wenziwao maneno ya kupambapamba ili kuwadanganya. Na kama Mola wako angalipenda wasingalifanya hayo, (angewalazimisha kwa nguvu kutii). Basi waache na uwongo wao.

وَكَذَٰلِكَ جَعَلْنَا لِكُلِّ نَبِىٍّ عَدُوًّا شَيَٰطِينَ ٱلْإِنسِ وَٱلْجِنِّ يُوحِى بَعْضُهُمْ إِلَىٰ بَعْضٍ زُخْرُفَ ٱلْقَوْلِ غُرُورًا وَلَوْ شَآءَ رَبُّكَ مَا فَعَلُوهُ فَذَرْهُمْ وَمَا يَفْتَرُونَ ﴿١١٢﴾

---

93. Yanatajwa yatakayowapata wabaya tangu saa ya kutoka roho mpaka saa ya kuhisabiwa.

94. Yanatajwa yatakayowakuta wabaya siku ya Kiama; kuwa (a) hawatakuwa na Mwombezi na (b) hata wakitoa kikomboleo gani, hakitakubaliwa.

| | |
|---|---|
| Sharia husema | Aso thawabu |
| Shida na mashaka | Yatamsibu |
| Shufaa ya Tumwal | Mahabubu |
| Huwa mbali naye | Na kumwegema. |

95-103. Baadhi ya sifa za Mwenyezi Mungu na neema zake juu ya viumbe vyake.

108. Hapa wanakatazwa Waislamu kutukana dini za watu wengine. Ukitaka kumbainishia mtu haki mbainishie kwa maneno mazuri, matamu, ya upole. Maneno mazuri humtoa nyoka pangoni.

109. Hapa wanakatishwa tamaa Waislamu juu ya makafiri hao washindani kuwa hawataamini hata wakiteremshiwa miujiza hiyo wanayoitaka.

111. Hapa inatajwa kuwa hata lau hao makafiri wakaidi wangeonyeshwa hiyo miujiza wanayoitaka, nao wasingeamini. Kama huko kutaka kwao (a) Wateremke Malaika wawape khabari kuwa kweli Nabii Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu; (b) Wafufuliwe waliokufa wawape habari hii pia; (c) Bali na kila kitu kije mbele yao kuwapa khabari hii.

112. Katika maelezo ya Aya hii waliyoifanya ni ya 113 wametia ukafiri wao mwengine wa kukataa viumbe vinavyoitwa majini. Kila Mwislamu anajua kuwa kuna Malaika na Binaadamu na Majini na wengineo. Na kila mmoja katika hao ameumbwa kwa vitu (zana) asivyoumbiwa mwenziwe. Malaika wameumbwa kwa Nuru. Binaadamu, Qurani yote nzima inasema, wameumbwa kwa Maji na kwa Udongo; na Majini wameumbwa kwa Moto. Qurani yote nzima imejaa katika kutaja kuumnbwa kwa Binaadamu kuwa wameumbwa (a) *Min Tyn* (b) *Min Sulaalatin Min Tyn (c) Min Turaabin (d) Min Salsaalin (e) Hamain (f) Min Main (g) Min Main Mahyn.* Na imejaa katika kutaja kuumbwa Majini na Mashetani (a) *Min Naar* (b) *Min Naaris Samuum.*

Wao wanajifanya wanajua hakika kuliko Mungu, wanamsuta Mwenyezi Mungu wanaandika hivi: "Maneno haya: *Watu na Majini,* ambayo yanapatikana katika Aya nyingi za Qurani hayaonyeshi viumbe vya namna mbili

113. Na ili zielekee kwa hayo (maneno yao) nyoyo za wale wasioamini Akhera na wayaridhie na ili wayachume wanayoyachuma.

وَلِتَصْغَىٰٓ إِلَيْهِ أَفْـِٔدَةُ ٱلَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِٱلْـَٔاخِرَةِ
وَلِيَرْضَوْهُ وَلِيَقْتَرِفُوا۟ مَا هُم مُّقْتَرِفُونَ ﴿١١٣﴾

114. (Sema): "Je, nimtafute hakimu asiyekuwa Mwenyezi Mungu (wa kunihukumu baina yangu na nyinyi), hali Yeye (Mwenyezi Mungu) ndiye aliyekuteremshieni Kitabu (hiki) kielezacho (kila kitu) waziwazi? (Na kishasema kuwa mimi nimo katika haki)." Na wale tuliowapa Kitabu wanajua ya kwamba kimeteremshwa na Mola wako kwa haki (ila wanapinga kwa inadi tu na uhasidi). Basi usiwe miongoni mwa wanaotia shaka.

أَفَغَيْرَ ٱللَّهِ أَبْتَغِى حَكَمًا وَهُوَ ٱلَّذِىٓ أَنزَلَ
إِلَيْكُمُ ٱلْكِتَٰبَ مُفَصَّلًا ۚ وَٱلَّذِينَ ءَاتَيْنَٰهُمُ
ٱلْكِتَٰبَ يَعْلَمُونَ أَنَّهُۥ مُنَزَّلٌ مِّن رَّبِّكَ بِٱلْحَقِّ ۖ فَلَا
تَكُونَنَّ مِنَ ٱلْمُمْتَرِينَ ﴿١١٤﴾

115. Na yametimia maneno ya Mola wako kwa kweli na uadilifu. Hakuna awezaye kuyabadilisha maneno Yake. Na Yeye ndiye asikiaye (na) ajuaye.

وَتَمَّتْ كَلِمَتُ رَبِّكَ صِدْقًا وَعَدْلًا ۚ لَّا مُبَدِّلَ
لِكَلِمَٰتِهِۦ ۚ وَهُوَ ٱلسَّمِيعُ ٱلْعَلِيمُ ﴿١١٥﴾

116. Na kama ukiwatii wengi katika (hawa) waliomo ulimwenguni watakupoteza na njia ya Mwenyezi Mungu. Hawafuati ila dhana tu, na hawakuwa ila ni wenye kuzua (tu basi).

وَإِن تُطِعْ أَكْثَرَ مَن فِى ٱلْأَرْضِ يُضِلُّوكَ
عَن سَبِيلِ ٱللَّهِ ۚ إِن يَتَّبِعُونَ إِلَّا ٱلظَّنَّ وَإِنْ هُمْ
إِلَّا يَخْرُصُونَ ﴿١١٦﴾

117. Bila shaka Mola wako ndiye anayewajua vyema wanaopotea na njia Yake, na ndiye anayewajua sana wanaoongoka.

إِنَّ رَبَّكَ هُوَ أَعْلَمُ مَن يَضِلُّ عَن سَبِيلِهِۦ ۖ
وَهُوَ أَعْلَمُ بِٱلْمُهْتَدِينَ ﴿١١٧﴾

118. Basi kuleni katika wale waliosomewa jina la Mwenyezi Mungu (wakachinjwa, si waliokufa wenyewe), ikiwa nyinyi mnaziamini Aya Zake.

فَكُلُوا۟ مِمَّا ذُكِرَ ٱسْمُ ٱللَّهِ عَلَيْهِ إِن كُنتُم بِـَٔايَٰتِهِۦ
مُؤْمِنِينَ ﴿١١٨﴾

119. Na kwa nini msile katika (wanyama) wale waliosomewa jina la Mwenyezi Mungu (naye amekuhalalishieni kula hivyo kwani havidhuru, kinyume cha vilivyokufa wenyewe)? Na amekubainishieni waziwazi alivyokuharimishieni, isipokuwa vile mnavyolazimika (kuvitumia kwa ajili ya njaa na mengineyo). Na hakika wengi wanapoteza (wengine) kwa matamanio yao bila ya kuwa na ilimu. Bila shaka Mola wako anawajua vyema wale warukao mipaka.

وَمَا لَكُمْ أَلَّا تَأْكُلُوا۟ مِمَّا ذُكِرَ ٱسْمُ ٱللَّهِ عَلَيْهِ
وَقَدْ فَصَّلَ لَكُم مَّا حَرَّمَ عَلَيْكُمْ إِلَّا
مَا ٱضْطُرِرْتُمْ إِلَيْهِ ۗ وَإِنَّ كَثِيرًا لَّيُضِلُّونَ بِأَهْوَآئِهِم
بِغَيْرِ عِلْمٍ ۗ إِنَّ رَبَّكَ هُوَ أَعْلَمُ بِٱلْمُعْتَدِينَ ﴿١١٩﴾

---

mbalimbali. Bali yanaonyesha watu wa namna mbili. *Ins* ni watu wote wa kawaida, na *Jinn* ni watu wakubwa wasiochanganyika ovyo na watu wengine na hawaonekani mara kwa mara." Kama huu si ukafiri, basi ni kitu gani? Mwenyezi Mungu Mwenyewe aseme ana viumbe alivyoviumba kwa kitu fulani akawaita Binaadamu; na ana viumbe alivyoviumba kwa kitu chingine, akaweta (akawaita) Majini. Wao wanamkaidi wanamwambia: "Huna viumbe namna mbili. Hao Majini ndio hao hao Insi—usijisifu bure kuwa umeumba viumbe namna mbili. Hao Majini ndio hao hao watu." Pimeni Waislamu mtazame hatari hii ya kuisoma tafsiri yao na maelezo yao (Mapotezo). Kwa nini hawakututajia hata mwanachuoni mmoja au mfasiri mmoja aliyesema kuwa Insi ndio Majini?

Yaliyo kweli ni kuwa wakati mwengine binaadamu unapozidi ubaya wake hunasibishiwa na viumbe wabaya kama Majini na Shetani na Mbwa na Nguruwe na Nyoka na kama hivi. Sio kuwa Binaadamu ndio Majini na ndio Mashetani. Basi na wawe ndio Mbwa na ndio Nyoka na ndio Nguruwe na ndio . . . Wanajua barabara kuwa hao

120. Na acheni dhambi zilizo dhahiri na zilizofichikana. Hakika wale wanaochuma dhambi watalipwa yale waliyokuwa wakiyachuma.

وَذَرُوا ظَاهِرَ الْإِثْمِ وَبَاطِنَهُ ۚ إِنَّ الَّذِينَ يَكْسِبُونَ الْإِثْمَ سَيُجْزَوْنَ بِمَا كَانُوا يَقْتَرِفُونَ ﴿١٢٠﴾

121. Wala msile katika wale wasiosomewa jina la Mwenyezi Mungu (yaani vilivyokufa wenyewe), maana (kula) huko ni uasi. Na kwa yakini mashetani wanawafunulia marafiki zao kubishana nanyi (katika mambo namna haya yasiyokuwa na maana). Na kama mkiwatii, mtakuwa washirikina.

وَلَا تَأْكُلُوا مِمَّا لَمْ يُذْكَرِ اسْمُ اللَّهِ عَلَيْهِ وَإِنَّهُ لَفِسْقٌ ۗ وَإِنَّ الشَّيَاطِينَ لَيُوحُونَ إِلَىٰ أَوْلِيَائِهِمْ لِيُجَادِلُوكُمْ ۖ وَإِنْ أَطَعْتُمُوهُمْ إِنَّكُمْ لَمُشْرِكُونَ ﴿١٢١﴾

122. Je, aliyekuwa maiti kisha tukamhuisha na tukamjaalia nuru, (yaani aliyekuwa kafiri kisha akasilimu); kwa (nuru) hiyo hutembea mbele za watu, atakuwa sawa na yule ambaye hali yake yuko gizani asiyeweza kutoka humo? Namna hivi wamepambiwa makafiri waliyokuwa wakiyafanya.

أَوَمَنْ كَانَ مَيْتًا فَأَحْيَيْنَاهُ وَجَعَلْنَا لَهُ نُورًا يَمْشِي بِهِ فِي النَّاسِ كَمَنْ مَثَلُهُ فِي الظُّلُمَاتِ لَيْسَ بِخَارِجٍ مِنْهَا ۚ كَذَٰلِكَ زُيِّنَ لِلْكَافِرِينَ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١٢٢﴾

123. Na kadhalika tulijaalia kila mji wakuu wao ndio waovu. Ikawa humo wanafanya hila (na vitimbi vya kuzuilia watu na dini ya Mwenyezi Mungu). Wala hawafanyii hila isipokuwa nafsi zao (kwani wanajidhuru wenyewe), lakini hawatambui.

وَكَذَٰلِكَ جَعَلْنَا فِي كُلِّ قَرْيَةٍ أَكَابِرَ مُجْرِمِيهَا لِيَمْكُرُوا فِيهَا ۖ وَمَا يَمْكُرُونَ إِلَّا بِأَنْفُسِهِمْ وَمَا يَشْعُرُونَ ﴿١٢٣﴾

124. Na zinapowafikia hoja husema: "Hatuwezi kuamini mpaka tupewe kama yale waliyopewa Mitume wa Mungu" (Yaani wapewe wahyi na wao). Mwenyezi Mungu ndiye ajuaye mahala anapoweka ujumbe wake (si kila mtu atapewa Utume tu). Itawafikia waovu hao dhila kubwa inayotoka kwa Mwenyezi Mungu na adhabu kali kwa sababu ya hila walizokuwa wakifanya.

وَإِذَا جَاءَتْهُمْ آيَةٌ قَالُوا لَنْ نُؤْمِنَ حَتَّىٰ نُؤْتَىٰ مِثْلَ مَا أُوتِيَ رُسُلُ اللَّهِ ۘ اللَّهُ أَعْلَمُ حَيْثُ يَجْعَلُ رِسَالَتَهُ ۗ سَيُصِيبُ الَّذِينَ أَجْرَمُوا صَغَارٌ عِنْدَ اللَّهِ وَعَذَابٌ شَدِيدٌ بِمَا كَانُوا يَمْكُرُونَ ﴿١٢٤﴾

---

Majini mbali na watu, lakini wanataka kuharibu tu itikadi za Waislamu kwani ndio kazi waliojiwekea kuifanya! Basi sharti wataifanya japo si kwa njia yenye maana.

Mara nyingi hutumika tamko la Shetani kwa kila aliye mbaya, akiwa Binadamu, akiwa Jini na akiwa Kiumbe kingine. Na hapa inaonyesha kuwa hao waovu hawakumshinda Mwenyezi Mungu, akitaka anaweza mara moja kuwazuilia wasifanye wanayoyafanya. Na angetaka angewaumba Kimalaika—hawawezi kufanya mabaya. Lakini amewaumba kibinadamu—amewapa uweza wa kukhiari kufanya mabaya au kufanya mema ili awalipe Pepo kwa kufanya mema na awalipe Moto kwa kufanya mabaya.

114. Wanatolewa akilini wanaokhitari hukumu isiyokuwa ya Mwenyezi Mungu.

116. Inaonyesha bahari mbaya. Nayo ni kuwa binaadamu wengi wamekhitari (a) Uovu kuliko wema na wamekhitari kufuata (b) ya Dhana kuliko ya yakini. Hapana raha wala kutengenekewa kuliko kufuata ya yakini. Basi ndio tunaambiwa kuwa: Usiwe mwendo wetu kutafuta kwenye wingi, bali uwe kutafuta kwenye Uwongofu.

Kama hivi kwetu sasa katika Uislamu, watu wengi kabisa wamo katika Mabidaa. Basi usitushutue wingi wao hao, tukawacha kwenye uongofu kwa kuwa wenyewe wachache. Wewe juu yako kufuata haki, sio mijitu laki ameyasema nafsi ya maneno haya Imamu Nawawy katika sahifa 72 ya kitabu chake — aladhkaar. Kwa Kiislamu Usafi *(quality)* ndio muhimu, sio wingi *(quantity)*.

118. Makafiri wakijidai kuwalaumu Waislamu ili wawadanganye wajinga; wakiwaambia Waislamu "Namna gani nyinyi mnakula mnachokiua nyinyi (yaani mnachokichinja), wala hamkubali kukila kilichouawa na Mwenyezi Mungu (yaani kilichokufa wenyewe)?"

125. Basi yule ambaye Mwenyezi Mungu anataka kumwongoza, hufungulia kifua chake Uislamu; na yule ambaye Mwenyezi Mungu anataka kumhukumu kupotea, hufanya kifua chake kizito kinaona taabu kubwa (kufuata huo Uislamu); kama kwamba anapanda mbinguni (kusikokuwa na pumzi). Namna hivi Mwenyezi Mungu anajaalia uchafu juu ya wale wasioamini.

فَمَن يُرِدِ اللَّهُ أَن يَهْدِيَهُ يَشْرَحْ صَدْرَهُ
لِلْإِسْلَامِ ۖ وَمَن يُرِدْ أَن يُضِلَّهُ يَجْعَلْ صَدْرَهُ
ضَيِّقًا حَرَجًا كَأَنَّمَا يَصَّعَّدُ فِي السَّمَاءِ ۚ كَذَٰلِكَ
يَجْعَلُ اللَّهُ الرِّجْسَ عَلَى الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿١٢٥﴾

126. Na hii (dini ya Uislamu) ndiyo njia ya Mola wako iliyonyoka. Bila shaka tumezipambanua Aya (namna hivi) kwa watu wenye kukumbuka.

وَهَٰذَا صِرَاطُ رَبِّكَ مُسْتَقِيمًا ۗ قَدْ فَصَّلْنَا
الْآيَاتِ لِقَوْمٍ يَذَّكَّرُونَ ﴿١٢٦﴾

127. (Watu wema) watapata nyumba ya salama kwa Mola wao. Naye ndiye mlinzi wao (mwenye kuwasimamia yao) kwa sababu ya yale waliyokuwa wakiyatenda.

لَهُمْ دَارُ السَّلَامِ عِندَ رَبِّهِمْ ۖ وَهُوَ وَلِيُّهُم بِمَا كَانُوا
يَعْمَلُونَ ﴿١٢٧﴾

128. Na (wakumbushe) siku atakapowakusanya wote, (awaambie):"Enyi makundi ya majini! Hakika nyinyi mmechukua wafuasi wengi katika wanaadamu." Na marafiki wao katika wanaadamu

وَيَوْمَ يَحْشُرُهُمْ جَمِيعًا يَا مَعْشَرَ الْجِنِّ قَدِ اسْتَكْثَرْتُم
مِّنَ الْإِنسِ ۖ وَقَالَ أَوْلِيَاؤُهُم مِّنَ الْإِنسِ رَبَّنَا

---

121. Wanaingia katika 'Wasiotajiwa jina la Mwenyezi Mungu' wanyama wanaochinjwa si kwa ajili ya kusema Mwenyezi Mungu na Mtume wake; japo wakipigwa Bismillahi. Basi wanakuwa NAJISI, NYAMAFU — haramu kuliwa; kama wanyama hawa:-

(a) Wanaochinjwa katika kaburi la Sharifu Fulani au Sheikh Fulani;
(b) Wanaochinjwa kwa ajili ya pepo Fulani;
(c) Kwa ajili ya jini wa mji kama yule anayezindikiwa mji, wakipita watu .... vijuzuu vyao wakisoma;
(d) Wanaochinjwa kwa ajili ya Shetani wa nyumba kila mwaka au pale wakati wa kutia msingi;
(e) Wanaochinjwa kwa ajili ya Shetani wa wazee;
(f) Wanaochinjwa kwa ajili ya Shetani wa kisima;
(g) Wanaochinjwa kwa ajili ya kukiushwa maiti, kukiushwa arusi, kukiushwa mgeni. Na kama haya.

Bali hata wale wanaochinjwa kwa ajili ya mashindano ya vyama kama vyama vya Maulidi au ngoma na mengineyo.

123. Kuonyesha kuwa mara nyingi wale wakubwa wa nchi ndio wanaokuwa mafisadi wa nchi hizi. Kwa kupapia kwao ukubwa hawatazami maslaha ya nchi, wanatazama maslaha ya nafsi zao. Hawana habari kuwa wanajidhuru wenyewe.

124. Miongoni mwa nyudhuru zao za upuzi za kukataa kumfuata Nabii Muhammad (s.a.w.) ni kusema: "Kwa nini hapewi miujiza tuliyotaka kwake," na kusema 'Na sisi natuletewe Wahy.' Na kusema vile vile 'Kwa nini akapewa huyu? Angepewa Bwana Fulani . . .' Basi ndio wanajibiwa hapa.

Katika hii Aya waliyoifanya ya 125 wamepenyeza kwa kijanja ukafiri wao wakaandika hivi: "Mungu hazungumzi na kila mtu, anazungumza na yule tu anayemwona kuwa anastahili, na anayemchagua."

Wametia haya ili kumgambia Utume huyo mtu wao, kwani huyo ana maneno — katika vitabu vyake vya ukafiri — anayoyasema kuwa ameambiwa na Mwenyewe Mwenyezi Mungu. Ukafiri wa kudai Utume baada ya Nabii Muhammad (s.a.w.) tumekwisha kutaja katika Marejezo ya Aya 7 ya *Suratul Faatiha* na Aya ya 4 ya *Suratul Baqarah*.

125. Mwenyezi Mungu amebainisha katika Aya nyingi kuwa huwaongoa wanaokubali kuongoka na anawaachia kupotea wasiotaka kuongoka. Siyo anafanya mambo ovyo ovyo tu—huyu amwongowe, yule ampoteze. Zikija Aya zinazodhanisha hivi (zilizotajwa kwa ufupi) inarejewa tafsiri yake katika zile Aya zilizotajwa kwa urefu. Inaambiwa katika ilimu ya tafsiri kuwa: *Yuhmalul Mutlaqu alal Muqayyad*. Kama (a) Aya ya 27 ya *Suratur Raad* na Aya ya 13 ya *Suratush Shuura* zinazosema kuwa "Mwenyezi Mungu humwongoa anayerejea kwake" (b) Aya ya 76 ya *Surati Maryam* na Aya ya 17 ya *Surat Muhammad* zinazosema kuwa: "Wanaokubali kuongoka, Mwenyezi Mungu anawazidisha uwongofu." Na kama hizi.

اسْتَمْتَعَ بَعْضُنَا بِبَعْضٍ وَبَلَغْنَا أَجَلَنَا الَّذِي
أَجَّلْتَ لَنَا ۚ قَالَ النَّارُ مَثْوَاكُمْ خَالِدِينَ فِيهَا إِلَّا
مَا شَاءَ اللَّهُ ۗ إِنَّ رَبَّكَ حَكِيمٌ عَلِيمٌ ﴿١٢٨﴾

(watawagombania) waseme: "Mola wetu! Tulinufaishana sisi na wao, na tumefikia muda wetu uliotuwekea." Basi (Mungu) atasema: "Moto ndio makazi yenu, mtakaa humo milele" ila apende Mwenyezi Mungu (kuwarehemu); hakika Mola wako ndiye Mwenye hikima (na) ndiye ajuaye.

وَكَذَٰلِكَ نُوَلِّي بَعْضَ الظَّالِمِينَ بَعْضًا بِمَا كَانُوا
يَكْسِبُونَ ﴿١٢٩﴾

129. Na vivi hivi tunawatia mapenzi baadhi ya madhalimu juu ya wengine (wakapiganiana) kwa sababu ya yale waliyokuwa wakiyachuma (kwa pamoja).

يَا مَعْشَرَ الْجِنِّ وَالْإِنسِ أَلَمْ يَأْتِكُمْ رُسُلٌ مِّنكُمْ
يَقُصُّونَ عَلَيْكُمْ آيَاتِي وَيُنذِرُونَكُمْ لِقَاءَ يَوْمِكُمْ
هَٰذَا ۚ قَالُوا شَهِدْنَا عَلَىٰ أَنفُسِنَا ۖ وَغَرَّتْهُمُ
الْحَيَاةُ الدُّنْيَا وَشَهِدُوا عَلَىٰ أَنفُسِهِمْ أَنَّهُمْ كَانُوا
كَافِرِينَ ﴿١٣٠﴾

130. (Siku ya Kiama wataambiwa): "Enyi makundi ya majini na wanaadamu! Je, hawajakufikieni Mitume miongoni mwenu kukubainishieni Aya zangu na kukuonyeni mkusanyo wa Siku yenu hii ya leo?" Watasema: "Tumeshuhudia juu ya nafsi zetu (kuwa sisi wabaya)". Na yaliwadanganya maisha ya dunia. Nao watajishuhudia wenyewe ya kwamba walikuwa makafiri.

ذَٰلِكَ أَن لَّمْ يَكُن رَّبُّكَ مُهْلِكَ الْقُرَىٰ بِظُلْمٍ
وَأَهْلُهَا غَافِلُونَ ﴿١٣١﴾

131. Hayo ni kwa sababu ya kuwa Mola wako hakuwa wa kuiangamiza miji kwa dhulma, hali wenyewe wameghafilika (hawakujiwa na Mitume wa kuwaonya).

وَلِكُلٍّ دَرَجَاتٌ مِّمَّا عَمِلُوا ۚ وَمَا رَبُّكَ بِغَافِلٍ
عَمَّا يَعْمَلُونَ ﴿١٣٢﴾

132. Na wote wana daraja sawa na yale waliyoyatenda. Na Mola wako si mwenye kughafilika na yale wanayoyatenda.

وَرَبُّكَ الْغَنِيُّ ذُو الرَّحْمَةِ ۚ إِن يَشَأْ يُذْهِبْكُمْ

133. Na Mola wako ndiye Mkwasi, Mwenye rehema. Kama akipenda atakuondoeni na kuweka

---

Na katika kinyume cha hizi, Mwenyezi Mungu anasema:- (a) Katika Aya ya 7 ya *Suratun Nahl* inayosema kuwa: "Mwenyezi Mungu hamwongoi anayepoteza (au kupotea mwenyewe)" (b) katika Aya ya 258 ya *Suratul Baqarah* na ya 86 ya *Surat Aali Imran* na ya 51 na ya 67 za *Suratul Maida* na ya 144 ya *Suratul An-am* na ya 19 na ya 109 za *Suratut Tauba* na ya 50 ya *Suratul Qasas* na ya 10 ya *Suratul Ahqaf* na ya 7 ya *Suratus Saf* na ya 5 ya *Suratul Jumua* zinazo sema kuwa: "Mwenyezi Mungu hawaongoi wanaodhulumu nafsi zao."

Na (c) Aya ya 86 ya *Surat Aali Imran* inayosema kuwa: "Vipi Mwenyezi Mungu atawaongoa wanaokufuru baada ya kuwadhihirikia ukweli wa dini ya Kiislamu?"

Na (d) Aya ya 27 ya *Surat Ibrahimu* inayosema kuwa: "Mwenyezi Mungu anawaachia wapotee wale wanaojidhulumu wenyewe nafsi zao.

Na (e) Aya ya 26 ya *Suratul Baqarah* inayosema kuwa: "(Mwenyezi Mungu) hawawachii kupotea . . . ila wale wenye kutoka na taa yake."

Na kama hizi nyingi kabisa. Si kweli hivyo kuwa Mwenyezi Mungu huwapoteza bure hao awatakao na akawaongoa bure awapendao

128. Wakubwa wa wabaya wa kibinaadamu watawapigania majini waliowapoteza wamwambie Mwenyezi Mungu kuwa kila mmoja katika wao amepata raha kwa mwenziwe. Wao majini wamepata raha ya kuona wamewapoteza wanaadamu, na wanaadamu wameona raha kwa hayo maasi waliokuwa wakiyafanya.

Wanaonyeshwa kuwa hawatatiwa Motoni kwa kuonewa: wamejistahikisha wenyewe hayo.

Katika Aya hizi walizozifanya ni za 129 na 131 wametaja tena ile itikadi yao kusema hakuna viumbe vinavyoitwa Majini. Tumekwisha kuyavunja haya katika Aya ya 112 ya hii *Suratul An-Am*.

Na Mwenyezi Mungu ametutajia katika Qurani dhahir shahir — kama ilivyo katika Aya ya 29 ya *Suratul Ahqaf;* na akateremsha Sura nzima akaiita *Suratul Jinn* — kumwambia Mtume na kutwambia sisi kuwa

wengine awapendao badala yenu, kama vile alivyokuumbeni katika uzazi wa watu wengine (sio wale walioangamizwa zama za Nabii Nuhu).

وَيَسْتَخْلِفْ مِنْ بَعْدِكُمْ مَّا يَشَآءُ كَمَآ أَنشَأَكُم مِّن ذُرِّيَّةِ قَوْمٍ ءَاخَرِينَ ۝

134. Bila shaka hayo mnayoahidiwa yatafika (tu); wala hamtaweza kuyashinda (mateso yake yatakapokujieni).

إِنَّ مَا تُوعَدُونَ لَءَاتٍ ۖ وَمَآ أَنتُم بِمُعْجِزِينَ ۝

135. Sema: "Enyi watu wangu! Tendeni yenu (mnayoyataka) kwa tamkini yenu (bila ya kuzuiliwa); na mimi (pia) natenda yangu. Mtajua ni nani atakuwa na makazi (mema) mwishoni. Hakika madhalimu hawatafuzu."

قُلْ يَٰقَوْمِ ٱعْمَلُوا۟ عَلَىٰ مَكَانَتِكُمْ إِنِّى عَامِلٌ ۖ فَسَوْفَ تَعْلَمُونَ مَن تَكُونُ لَهُۥ عَٰقِبَةُ ٱلدَّارِ ۗ إِنَّهُۥ لَا يُفْلِحُ ٱلظَّٰلِمُونَ ۝

136. Na wamemfanyia Mwenyezi Mungu sehemu katika mimea aliyoiumba (Mwenyewe) na katika wanyama (aliowaumba Mwenyewe), na husema: "Hii ni sehemu ya Mwenyezi Mungu," kwa madai yao (tu), "Na hii ni ya (wale) tunaowashirikisha na Mungu." Basi vile walivyowakusudia waungu wao havifiki kwa Mwenyezi Mungu, na vilivyokuwa vya Mwenyezi Mungu hivyo hufika kwa waungu wao. Ni mabaya kabisa wanayoyahukumu.

وَجَعَلُوا۟ لِلَّهِ مِمَّا ذَرَأَ مِنَ ٱلْحَرْثِ وَٱلْأَنْعَٰمِ نَصِيبًا فَقَالُوا۟ هَٰذَا لِلَّهِ بِزَعْمِهِمْ وَهَٰذَا لِشُرَكَآئِنَا ۖ فَمَا كَانَ لِشُرَكَآئِهِمْ فَلَا يَصِلُ إِلَى ٱللَّهِ ۖ وَمَا كَانَ لِلَّهِ فَهُوَ يَصِلُ إِلَىٰ شُرَكَآئِهِمْ ۗ سَآءَ مَا يَحْكُمُونَ ۝

137. Na namna hivi waungu wao hao wanaowashirikisha (na Mwenyezi Mungu)

وَكَذَٰلِكَ زَيَّنَ لِكَثِيرٍ مِّنَ ٱلْمُشْرِكِينَ قَتْلَ أَوْلَٰدِهِمْ

---

Mwenyezi Mungu alimletea Nabii Muhammad Majini kuja kusikiliza anayoyasema, na wakaamini na wakenda kuwakhubiri Majini wenziwao. Wakasilimu waliosilimu na wakakataa waliokataa, kama kwa Binaadamu vile vile. Ukafiri katika jambo hili si la uficho kwani hakuna Mwislamu yo yote asiyeitakidi kuwa viumbe vinavyoitwa Majini — wao ni viumbe mbali si Binaadamu, na wameumbwa kwa kitu chengine sicho kile walichoumbiwa Binaadamu. Hakuna Mwislamu anayekanusha haya; basi hii ni alama moja ya ukafiri wao kumsuta Mwenyezi Mungu wakamfanya hajui, wao ndio wanaojua. Basi sisi hatutamwacha Mwenyezi Mungu tukawafuata wao. Huo ni ukafiri uliotia maji maziwani.

131. Mwenyezi Mungu hawatesi watu kabla hawajawajia Mtume. Hawatesi kwa yale mambo ambayo hayawezi kufahamika kwa akili zao pasina kufundishwa na Mtume; kama kusali, kufunga. Atawatesa kwa yale wanayoweza kuyafahamu kuwa mabaya — kama mtu kumdhulumu mwenziwe — nao wakayafanya.

133. Wanaadamu wanaoishi sasa wanatokana na wale watoto watatu wa Nabii Nuhu waliosalimika na tufani ya safari hiyo na wakazaa. Wale wengine waliosalimika pamoja nao hawakuzaa. Ama wale makafiri wamepotea kabisa — hapana hata kizazi chao.

135. Kuonyesha kuwa kila binaadamu amepewa huria (Uhuru) ya kufanya au kuwacha; wasije wakasema wameonewa, na kuonyesha kuwa wabaya hawatapata ila mabaya.

136. Makafiri wakulima hapo zamani wakati wanapopanda konde zao hutia mipaka vipande viwili vitatu wakasema. "Kipande hiki cha Mwenyezi Mungu" — yaani pato lake watalitumia katika kuwapa masikini, mayatima na wahitaji na walio namna hiyo. Na wakasema 'Kipande hiki cha wale (masanamu) tunaowashirikisha na Mwenyezi Mungu' — yaani pato lake lipewe wale wanaowatunza hao masanamu na kuwalinda.

Basi ikitokea bahati ya kuharibika (au kutopata mavuno mazuri) ile sehemu ya masanamu, huichukua ile sehemu waliosema kuwa ya Mwenyezi Mungu wakafanya ndiyo sehemu ya masanamu, na sehemu ya Mwenyezi Mungu ikawa ile mbovu mbovu iliyoharibika.

Na ikitokea bahati ya kuharibika ile sehemu waliyosema kuwa ya Mwenyezi Mungu, hawaishughulikii cho chote, huiachilia mbali, kama kwamba wanaonyesha kuwa hao masanamu ni bora kuliko Mwenyewe Mwenyezi Mungu.

Na wakiwa na wanyama wao ni vivi hivi pia. Baadhi yao husema: 'Kizazi cha hawa ni sehemu ya Mungu na kizazi cha hawa ni sehemu ya masanamu.' Basi kikifa cha masanamu au kisipobariki uzuri hubadili kwa kile walichosema kuwa ni cha Mungu.

شُرَكَآؤُهُمْ لِيُرْدُوهُمْ وَلِيَلْبِسُوا عَلَيْهِمْ دِينَهُمْ ۖ
وَلَوْ شَآءَ ٱللَّهُ مَا فَعَلُوهُ ۖ فَذَرْهُمْ وَمَا يَفْتَرُونَ ﴿١٣٧﴾

wamewapambia wengi katika washirikina hao kuwaua watoto wao, ili kuwaangamiza na kuwavurugia dini yao. Na kama Mwenyezi Mungu angependa wasingalifanya hayo. Basi waache na hayo wanayoyatunga.

وَقَالُوا هَٰذِهِۦٓ أَنْعَٰمٌ وَحَرْثٌ حِجْرٌ لَّا يَطْعَمُهَآ
إِلَّا مَن نَّشَآءُ بِزَعْمِهِمْ وَأَنْعَٰمٌ حُرِّمَتْ ظُهُورُهَا
وَأَنْعَٰمٌ لَّا يَذْكُرُونَ ٱسْمَ ٱللَّهِ عَلَيْهَا ٱفْتِرَآءً
عَلَيْهِ ۚ سَيَجْزِيهِم بِمَا كَانُوا يَفْتَرُونَ ﴿١٣٨﴾

138. Nao husema (vile vile): "Wanyama hawa (wamekatazwa), na mimea hii imekatazwa, hawatawala ila wale tuwapendao." Kwa madai yao (tu wanasema haya; wanamsingizia uwongo Mwenyezi Mungu kuwa kawaamrisha hayo). Na (husema pia): "Wanyama hawa migongo yao imeharimishwa (kupandwa)." Na wanyama wengine hawalitaji jina la Mwenyezi Mungu juu yao (wakati wa kuwachinja yasije yakakasirikia masanamu yao) — Wanamzulia uwongo (tu Mwenyezi Mungu). Atawalipa kwa haya waliyokuwa wakiyatunga.

وَقَالُوا مَا فِى بُطُونِ هَٰذِهِ ٱلْأَنْعَٰمِ خَالِصَةٌ
لِّذُكُورِنَا وَمُحَرَّمٌ عَلَىٰٓ أَزْوَٰجِنَا ۖ وَإِن يَكُن مَّيْتَةً
فَهُمْ فِيهِ شُرَكَآءُ ۚ سَيَجْزِيهِمْ وَصْفَهُمْ ۚ إِنَّهُۥ
حَكِيمٌ عَلِيمٌ ﴿١٣٩﴾

139. Na husema: (kadhalika) "Waliomo matumboni mwa wanyama hawa ni kwa ajili ya wanaume wetu tu, na wameharimishwa kwa wake wetu." Lakini ikiwa nyamafu basi wanashirikiana (na wanawake makafiri wakala hao nyamafu). Hakika atawalipa maelezo yao (ya uwongo hayo). Bila shaka Yeye ni Mwenye hikima na mjuzi.

قَدْ خَسِرَ ٱلَّذِينَ قَتَلُوٓا أَوْلَٰدَهُمْ سَفَهًۢا بِغَيْرِ
عِلْمٍ وَحَرَّمُوا مَا رَزَقَهُمُ ٱللَّهُ ٱفْتِرَآءً عَلَى ٱللَّهِ ۚ
قَدْ ضَلُّوا وَمَا كَانُوا مُهْتَدِينَ ﴿١٤٠﴾

140. Hakika wamekhasirika wale ambao wamewaua watoto wao kwa upumbavu pasipo kujua, na wakaharimisha alivyowaruzuku Mwenyezi Mungu (kama vile vilivyotajwa) kwa kumtungia uwongo Mwenyezi Mungu. Bila shaka wamepotea wala hawakuwa wenye kuongoka.

وَهُوَ ٱلَّذِىٓ أَنشَأَ جَنَّٰتٍ مَّعْرُوشَٰتٍ وَغَيْرَ
مَعْرُوشَٰتٍ وَٱلنَّخْلَ وَٱلزَّرْعَ مُخْتَلِفًا أُكُلُهُۥ
وَٱلزَّيْتُونَ وَٱلرُّمَّانَ مُتَشَٰبِهًا وَغَيْرَ مُتَشَٰبِهٍ ۚ

141. Naye (Mwenyezi Mungu) ndiye aliyeiumba miti inayoegemezwa (katika chanja katika kuota kwake), na isiyoegemezwa, na (akaumba) mitende na mimea yenye matunda mbalimbali, na (akaumba) mizaituni na mikomamanga inayofanana na isiyofanana. Kuleni matunda yake inapotoa

*N.B*.–Na kuna baadhi ya Waislamu wengine wanakaribia kuwa kama hawa, lakini hilo lao si la ukafiri ila ni la kuacha MUHIMU wakashughulikia lisilokuwa muhimu. Kama wanaoshughulikia kusoma na kusomesha Maulidi wakaacha kujenga na kuitengeneza misikiti na vyuo vya Qurani na Ilimu na kuwasaidia hao Wanafunzi na *Talabatul Ilm*. Wakaona kuwa kusoma Maulidi na kufanya Ziara ni bora kuliko haya. Nani atakayesema kuwa haya ni bora kuliko yale ila anayetaka kupoteza watu na kuurejesha mwendo wa dini nyuma? Basi khiari zao. Nawawapoteze watu! Wataona wenyewe Kiama! Na hao watu nawakubali tu kupotezwa na waache aliyoyasema Mwenyezi Mungu na Mtume wake, wafuate porojo! Wataona wenyewe pia. Wanakubalia nini kupotezwa?

Siku ya Kiama waliopotezwa watawatilia chonza kwa Mwenyezi Mungu wale waliowapoteza waseme: "Eee Mola wetu! Wenye kutusababishia haya wazidishie mara nyingi hiyo adhabu yao ya Moto (kwani ndio waliotupoteza)." Na Mwenyezi Mungu atawajibu kuwa: "Kila mmoja ana adhabu mara mbili; (wao kwa kujipoteza wenyewe na kupoteza watu; na nyinyi kwa kule kukubali kupotezwa na mkapotea).

137. Makafiri walikuwa wakiwatoa mihanga watoto wao kuwapa masanamu yao; wakiona ni kheri hiyo wanafanya.

138. Na hawa wanaojipa Uislamu wanayo baadhi ya haya. Kama vile wapunga pepo. Kuna wanaojidai kuwa

matunda; na toeni haki yake siku ya kuvunwa kwake (kwa kuwapa masikini na jamaa na majirani na wengineo). Wala msitumie kwa fujo, hakika Yeye Mwenyezi Mungu) hawapendi watumiyao kwa fujo

كُلُوا مِن ثَمَرِهِۦٓ إِذَآ أَثْمَرَ وَءَاتُوا حَقَّهُۥ يَوْمَ حَصَادِهِۦ
وَلَا تُسْرِفُوٓا إِنَّهُۥ لَا يُحِبُّ الْمُسْرِفِينَ ﴿١٤١﴾

142. Na katika wanyama (akakuumbieni) wale wabebao mizigo na wanaopandwa. Kuleni katika alivyokuruzukuni Mwenyezi Mungu, wala msifuate nyayo za Shetani; kwa yakini yeye ni adui yenu dhahiri

وَمِنَ الْأَنْعَامِ حَمُولَةً وَفَرْشًا كُلُوا مِمَّا رَزَقَكُمُ
اللَّهُ وَلَا تَتَّبِعُوا خُطُوَٰتِ الشَّيْطَٰنِ إِنَّهُۥ لَكُمْ
عَدُوٌّ مُّبِينٌ ﴿١٤٢﴾

143. (Amekuumbieni) namna nane za wanyama (hawa; madume na majike). Wawili katika kondoo, (dume na jike); na wawili katika mbuzi, (dume na jike). Sema (Uwaambie): "Je, ameharimisha yote madume mawili (ya kondoo na mbuzi) au majike mawili, au waliomo matumboni mwa majike yote mawili? Niambieni kwa ilimu ikiwa nyinyi mnasema kweli

ثَمَٰنِيَةَ أَزْوَٰجٍ مِّنَ الضَّأْنِ اثْنَيْنِ وَمِنَ الْمَعْزِ
اثْنَيْنِ قُلْ ءَآلذَّكَرَيْنِ حَرَّمَ أَمِ الْأُنثَيَيْنِ أَمَّا
اشْتَمَلَتْ عَلَيْهِ أَرْحَامُ الْأُنثَيَيْنِ نَبِّـُٔونِى بِعِلْمٍ
إِن كُنتُمْ صَٰدِقِينَ ﴿١٤٣﴾

144. Na wawili katika ngamia, (dume na jike); na wawili katika ng'ombe, (dume na jike). Sema: "Je, ameharimisha yote madume mawili au majike mawili, au waliomo matumboni mwa yote majike? Au, nyinyi mlikuwako Mwenyezi Mungu alipokuusieni haya?" Basi ni nani dhalimu mkubwa kuliko yule aliyemtungia Mwenyezi Mungu uwongo ili kuwapoteza watu bila ya ilimu? Hakika Mwenyezi Mungu hawaongozi watu madhalimu.

وَمِنَ الْإِبِلِ اثْنَيْنِ وَمِنَ الْبَقَرِ اثْنَيْنِ
قُلْ ءَآلذَّكَرَيْنِ حَرَّمَ أَمِ الْأُنثَيَيْنِ أَمَّا اشْتَمَلَتْ
عَلَيْهِ أَرْحَامُ الْأُنثَيَيْنِ أَمْ كُنتُمْ شُهَدَآءَ إِذْ
وَصَّىٰكُمُ اللَّهُ بِهَٰذَا فَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنِ افْتَرَىٰ
عَلَى اللَّهِ كَذِبًا لِّيُضِلَّ النَّاسَ بِغَيْرِ عِلْمٍ إِنَّ اللَّهَ
لَا يَهْدِى الْقَوْمَ الظَّٰلِمِينَ ﴿١٤٤﴾

---

wao wanapunga pepo makafiri. Basi wanaponywisha damu ya pepo kafiri wanakataza kutaja jina la Mwenyezi Mungu wakati wa kuwachinja wanyama hao. Na ati kuna magonjwa ambayo haifai mgonjwa wake kusomewa kisomo kilichoshikamana na jina la Mwenyezi Mungu. Badala ya kuwa jina la Mungu dawa, wao wanaliona ni la kuleta shakawa; Wamejifanya wao na makafiri sawa. Tena vile vile wanawalewesha hao wanaowapunga hao wanaowaita pepo wa kikafiri! Wanawalewesha hivi vileweshaji vya Kizungu.

139. Na wanaume wa kinchi zetu hizi walipokuwa watu kizani waliwaharimishia wanawake baadhi ya vyakula pia kuwa hivyo ni vya wanaume si vya wanawake. Vijiwanawake vizee vilivyosalia bado—vinakula chumvi mpaka leo—havikubali kula firigisi ya kuku. Wanasema 'Hiyo hupelekwa barazani kwa wenyewe wanaume.' Bali walifundishwa kutokula mpaka weshe kula wanaume, kirejee chakula barazani.

141. Anakumbusha hapa Mwenyezi Mungu neema alizowapa viumbe vyake kwa ajili ya mimea. Kisha anaamrisha hao wenye hiyo mimea watoe sehemu ya KILA wanachokivuna wawape wasiokuwa nayo, khasa wakiwa jamaa na majirani; basi seuze watu wao wa majumbani. Kuna watu wengine wanawakhinisha sana watu wao majumbani. Ni jambo baya kabisa.

UBAKHILI si kitu kinachopendwa na Uislamu. Na UBADHIRIFU (ufujaji) pia ni vivyo hivyo.

Ndiyo maana Mwenyezi Mungu akafuatishia hapa akasema:- "Wala msitumie kwa fujo . . ."

Na dasturi ya nchi zetu hizi wakishapata kitu basi watazukiwa na shughuli mia na moja ambazo hapana moja katika hizo iliyo ya dharura; lakini basi tu. Hizo fedha walizonazo zinawawasha wanataka wazitoe.

Wakati huo huzuka habari ya '1) Kutia watoto jandoni; (2) Kuoa mke wa pili au zaidi; (3) Kutokea bibie ukumbini; (4, Kupungwa pepo; (5) Kusomea khitima wazee; (6) Kuvutiwa Tahalili; (7) Kuwafanyia akika watoto walio kufa; hali ya kuwa akika husuniwa kwa kuzaliwa mtoto si kwa kufa kwake; (8) Kusoma Maulidi makubwa; (9) Maziyara; (10) Kufanya Riya za kuhiji tena na tena; 11) Kufanya karamu za bure zisizokuwa na sababu yo yote ila kule kuwashwa tu na hizo pesa; utadhani kunguni wakali au viroboto na chawa.

145. Sema: "Sioni katika yale niliyofunuliwa mimi (niliyoletewa wahyi; sioni) kitu kilichoharimishwa kwa mlaji kukila isipokuwa kiwe ni mzoga au damu inayomwagika au nyama ya nguruwe, kwani hivyo ni uchafu; au kile ambacho kwa kukhalifiwa amri ya Mwenyezi Mungu kimechinjwa kwa jina la asiyekuwa Mwenyezi Mungu. Lakini aliyelazimika (kula kwa ajili ya njaa au mengine) pasipo kupenda wala kuruka mipaka, basi (huyo atasamehewa, kwani) Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu.

قُل لَّآ أَجِدُ فِى مَآ أُوحِىَ إِلَىَّ مُحَرَّمًا عَلَىٰ طَاعِمٍ
يَطْعَمُهُۥٓ إِلَّآ أَن يَكُونَ مَيْتَةً أَوْ دَمًا مَّسْفُوحًا
أَوْ لَحْمَ خِنزِيرٍ فَإِنَّهُۥ رِجْسٌ أَوْ فِسْقًا أُهِلَّ لِغَيْرِ ٱللَّهِ
بِهِۦ ۚ فَمَنِ ٱضْطُرَّ غَيْرَ بَاغٍ وَلَا عَادٍ فَإِنَّ رَبَّكَ
غَفُورٌ رَّحِيمٌ ١٤٥

146. Na kwa wale walio Mayahudi tuliharimisha kila (mnyama). Mwenye kucha. Na katika ng'ombe na kondoo na mbuzi tukawaharimishia shahamu (mafuta) yao isipokuwa ile iliyobeba migongo yake (wanyama hao) au (iliyobeba) matumbo au ile iliyogandamana na mifupa. Tuliwalipa hivyo kwa sababu ya uasi wao. Na bila shaka Sisi ndio wakweli (Sio wao wanaojidai kuwa Mungu hakuharimisha haya kwa ajili ya ubaya wao; lakini wenyewe tu wazee wa Kiyahudi walijiharimishia haya, na wao chipukizi zao wakafuata).

وَعَلَى ٱلَّذِينَ هَادُوا۟ حَرَّمْنَا كُلَّ ذِى ظُفُرٍ ۖ وَمِنَ
ٱلْبَقَرِ وَٱلْغَنَمِ حَرَّمْنَا عَلَيْهِمْ شُحُومَهُمَآ إِلَّا مَا
حَمَلَتْ ظُهُورُهُمَآ أَوِ ٱلْحَوَايَآ أَوْ مَا ٱخْتَلَطَ بِعَظْمٍ ۚ
ذَٰلِكَ جَزَيْنَٰهُم بِبَغْيِهِمْ ۖ وَإِنَّا لَصَٰدِقُونَ ١٤٦

147. Wakidumu kukukadhibisha sema: "Mola wenu ana rehema nyingi (ndiyo maana anakawilisha kukuteseni); na (juu ya hivi) adhabu Yake haizuiliwi (isifike) kwa watu waovu."

فَإِن كَذَّبُوكَ فَقُل رَّبُّكُمْ ذُو رَحْمَةٍ وَٰسِعَةٍ
وَلَا يُرَدُّ بَأْسُهُۥ عَنِ ٱلْقَوْمِ ٱلْمُجْرِمِينَ ١٤٧

148. Wanaomshirikisha Mwenyezi Mungu watasema: "Angalipenda Mwenyezi Mungu tusingalimshirikisha sisi wala baba zetu, wala tusingaliharimisha cho chote. (Basi haya tunayoyafanya anayapenda Mwenyezi Mungu)." Vivi hivi walikadhibisha waliokuwa kabla yao mpaka wakaonja adhabu yetu. Sema: "Je, nyinyi mnayo ilimu (katika haya mnayoyasema) mtutolee (kuwa Mwenyezi Mungu amekuamrisheni kufanya mabaya haya? Uwongo tu)? Nyinyi hamfuati ila dhana tu, wala hamsemi ila uwongo tu."

سَيَقُولُ ٱلَّذِينَ أَشْرَكُوا۟ لَوْ شَآءَ ٱللَّهُ مَآ أَشْرَكْنَا
وَلَآ ءَابَآؤُنَا وَلَا حَرَّمْنَا مِن شَىْءٍ ۚ كَذَٰلِكَ
كَذَّبَ ٱلَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ حَتَّىٰ ذَاقُوا۟ بَأْسَنَا ۗ
قُلْ هَلْ عِندَكُم مِّنْ عِلْمٍ فَتُخْرِجُوهُ لَنَآ ۖ
إِن تَتَّبِعُونَ إِلَّا ٱلظَّنَّ وَإِنْ أَنتُمْ إِلَّا تَخْرُصُونَ ١٤٨

---

Na mambo ya kheri mangapi yako ya kutumilia pesa hizo ambayo yatamfaa yeye na watu wake na uma wake hapa duniani, yaje yampe faida kubwa kabisa Akhera. Nayo hayashughulikii.

Wao ima watakuwa mabakhili wasijinufaishe wao wala watu wao wala Uma. Au watakuwa wafujaji wawadhuru wote hao. Lakini kuwa katikati—mahali aliposema Mwenyezi Mungu, na kila mwenye akili akapoana ndipo—hawawi kabisa. Basi mwendo gani huo usiokuwa wa Kiislamu wala wa kiakili, wanaoufuata wao!

Wakirithi huwa namna hii hii. Wakivuna pia vivi hivi. Na kadhalika wanapopokea mishahara yao.

142. Waarabu walikuwa wakiharimisha kula baadhi ya wanyama kama tulivyoona. Basi akaambiwa Mtume awwambie maneno haya.

143. Basi vipi kusema kuwa "Hawa haramu na hawa halali" na hali ya kuwa wote wanatokana na dume na jike? Vipi hawa watakuwa haramu na hawa wanakuwa halali? Ima wote wawe haramu au wote wawe halali.

149. Sema: "Basi Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye hoja ya kweli (juu yenu); na kama angalipenda angekuongozeni nyinyi nyote," (muwe kama Malaika, hamna matamanio. Lakini amekupeni akili na matamanio ili mpigane na hayo matamanio. Mkiyashinda muingie Peponi kwa daraja kubwa kuliko za Malaika. Na yakikushindeni muingie Motoni kwa udhalilifu kuliko wanyama)."

قُلْ فَلِلَّهِ الْحُجَّةُ الْبَالِغَةُ ۚ فَلَوْ شَاءَ لَهَدَاكُمْ
أَجْمَعِينَ ﴿١٤٩﴾

150. Sema: "Leteni mashahidi wenu wanaoweza kushuhudia kuwa Mwenyezi Mungu ameharimisha (wanyama) hawa (mnaosema kuwa Mwenyezi Mungu amewaharimisha)." Basi wakitoa ushahidi (wa uwongo huo), wewe usishuhudie pamoja nao, wala usifuate matamanio ya wale waliokadhibisha Aya zetu na wale wasioiamini Akhera na ambao wanawafanya (masanamu) sawa na Mola wao (Mwenyezi Mungu).

قُلْ هَلُمَّ شُهَدَاءَكُمُ الَّذِينَ يَشْهَدُونَ أَنَّ اللَّهَ
حَرَّمَ هَٰذَا ۚ فَإِن شَهِدُوا فَلَا تَشْهَدْ مَعَهُمْ ۚ
وَلَا تَتَّبِعْ أَهْوَاءَ الَّذِينَ كَذَّبُوا بِآيَاتِنَا وَالَّذِينَ لَا
يُؤْمِنُونَ بِالْآخِرَةِ وَهُم بِرَبِّهِمْ يَعْدِلُونَ ﴿١٥٠﴾ ع

151. Sema (waambie): "Njooni nikusomeeni aliyokuharimishieni Mola wenu (na aliyokuamrisheni; si yale ya uwongo mnayojidai nyinyi kuwa Mungu amekuamrisheni): ya kwamba msimshirikishe na cho chote. Na wafanyieni wema wazazi wenu. Wala msiwaue watoto wenu kwa sababu ya umasikini. Sisi tutakupeni riziki nyinyi na wao pia. Wala msikaribie mambo maovu, yaliyo dhahiri na yaliyo siri. Wala msimwue mtu ambaye Mwenyezi Mungu ameharimisha (kuuawa), ila ikiwa (imetokea) haki (ya kuuawa). Amekuusieni haya ili mpate kuyatia akilini" (myafuate).

قُلْ تَعَالَوْا أَتْلُ مَا حَرَّمَ رَبُّكُمْ عَلَيْكُمْ ۖ أَلَّا تُشْرِكُوا
بِهِ شَيْئًا ۖ وَبِالْوَالِدَيْنِ إِحْسَانًا ۖ وَلَا تَقْتُلُوا
أَوْلَادَكُم مِّنْ إِمْلَاقٍ ۖ نَّحْنُ نَرْزُقُكُمْ وَإِيَّاهُمْ ۖ
وَلَا تَقْرَبُوا الْفَوَاحِشَ مَا ظَهَرَ مِنْهَا وَمَا بَطَنَ ۖ
وَلَا تَقْتُلُوا النَّفْسَ الَّتِي حَرَّمَ اللَّهُ إِلَّا بِالْحَقِّ ۚ
ذَٰلِكُمْ وَصَّاكُم بِهِ لَعَلَّكُمْ تَعْقِلُونَ ﴿١٥١﴾

---

145. Hapa wanatajwa wale wanyama waliohariminshwa kuwala kama walivyotajwa mara nyingi. Na inatajwa vile vile—kama ilivyotajwa mara nyingi—kuwa kwa dharura kubwa huhalalishwa kula hivyo vilivyoharimishwa kama (a) Njaa kubwa ya kumtoa mtu roho au (b) Ugonjwa mkubwa ambao madaktari wakubwa wa kutegemewa wamesema kuwa kitu hicho ndiyo dawa, kama vile kutiwa mtu damu ya mtu mwengine.

*N.B.*—Wala mtu akitiwa damu ya mtu mwengine hawi ndugu wa mtu huyo. Watu wengi huitikadi kuwa wanaotiana damu wanakuwa ndugu, kwa hivyo wanamzuilia mume asitoe damu yake kutiwa mkewe au mke kutoa damu yake kutiwa mumewe. Hayo si maneno yaliyosemwa na wenye ilimu. Hayo ni porojo la mdomo tu. Na inafaa mtu kutiwa jicho la maiti au moyo wake au kiungo chake chengine alicho kikubali mwenyewe maiti kabla ya kufa au wakikubali jamaa zake.

146. Yanatajwa baadhi ya yaliyowafika Mayahudi kwa ubaya wao.

148. Tumeyabainisha haya katika Aya ya 125 ya Sura hii.

151. Waarabu wengine walikuwa wakiuwa watoto wao wanapokuwa mafakiri au wanapochelea kuwa watakuwa mafakiri kwa hiyo idadi nyingi ya watoto wanaowajia. Basi huwaua wanaowaona kuwa hao wamezidi kuliko uweza wao.

Na waliokuwa wakiuawa ni watoto wanawake tu kwani wakiwaona kuwa hawataweza kuwasaidia katika taabu za maisha. Ama watoto wanaume wakiwalea. Wakifurahiwa sana kwa kuzaa watoto wanaume na wakihuzunika sana kwa kuzaa watoto wanawake.

Na iliposemwa 'Wala msikaribie mambo maovu,' ni kuonyesha kuwa maovu inataka mtu asiyefanye wala asikaribie mahala yanapofanywa kwani moyo hupanda zaidi Uibilisi wake wakati unapoona mahala penye mabaya au kuyaona hayo mabaya yanafanywa.

152. "Wala msikaribie mali ya yatima, isipokuwa kwa njia bora (ya kumtengenezea hicho chake) mpaka afike baleghe yake (umpe mwenyewe). Na kamilisheni vipimo vya vibaba na mizani kwa uadilifu — hatumkalifishi mtu ila kwa kadiri ya uweza wake (Na haya yanawezekana). Na msemapo (katika shahada na penginepo) semeni kwa insafu ingawa ni jamaa; (usimpendelee kwa ajili ya ujamaa uliyo baina yenu au kwa ajili ya kukupa mrungura. Na mambo kama haya). Na tekelezeni ahadi ya Mwenyezi Mungu. Amekuusieni haya ili mpate kukumbuka"

وَلَا تَقْرَبُوا مَالَ الْيَتِيمِ إِلَّا بِالَّتِي هِيَ أَحْسَنُ حَتَّىٰ
يَبْلُغَ أَشُدَّهُ ۚ وَأَوْفُوا الْكَيْلَ وَالْمِيزَانَ
بِالْقِسْطِ ۚ لَا نُكَلِّفُ نَفْسًا إِلَّا وُسْعَهَا ۚ وَإِذَا
قُلْتُمْ فَاعْدِلُوا وَلَوْ كَانَ ذَا قُرْبَىٰ ۚ وَبِعَهْدِ اللَّهِ
أَوْفُوا ۚ ذَٰلِكُمْ وَصَّاكُمْ بِهِ لَعَلَّكُمْ
تَذَكَّرُونَ ﴿١٥٢﴾

153. (Na sema uwaambie): "Na kwa hakika hii ndiyo njia yangu iliyonyoka. Basi ifuateni wala msifuate njia nyingine, zikakutengeni mbali na njia Yake (Mwenyezi Mungu). Amekuusieni haya ili mpate kujilinda (na kila mabaya ya duniani na Akhera).

وَأَنَّ هَٰذَا صِرَاطِي مُسْتَقِيمًا فَاتَّبِعُوهُ ۖ
وَلَا تَتَّبِعُوا السُّبُلَ فَتَفَرَّقَ بِكُمْ عَنْ سَبِيلِهِ ۚ
ذَٰلِكُمْ وَصَّاكُمْ بِهِ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ ﴿١٥٣﴾

154. Tena tulimpa Musa Kitabu kwa kutimiza (neema) juu ya yule aliyefanya wema, na kuwa maelezo ya kila kitu, na uwongozi na rehema, ili wapate kuamini mkutano wao na Mola wao.

ثُمَّ آتَيْنَا مُوسَى الْكِتَابَ تَمَامًا عَلَى الَّذِي أَحْسَنَ
وَتَفْصِيلًا لِكُلِّ شَيْءٍ وَهُدًى وَرَحْمَةً لَعَلَّهُمْ
بِلِقَاءِ رَبِّهِمْ يُؤْمِنُونَ ﴿١٥٤﴾

155. Na hii (Qurani) ni Kitabu tulichokiteremsha (kwenu), kilicho na baraka nyingi. Basi kifuateni na muwe wacha Mungu ili mrehemewe

وَهَٰذَا كِتَابٌ أَنْزَلْنَاهُ مُبَارَكٌ فَاتَّبِعُوهُ وَاتَّقُوا
لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُونَ ﴿١٥٥﴾

---

Mlevi yo yote hakulewa ila baada ya kuwakaribia hao walevi. Wala mwizi mkubwa hakuiiba ila baada ya kuchanganyika na hao wezi. Na mengineyo ndiyo vivyo hivyo. Ndiyo maana ikaambiwa hapa Msiyakaribie mambo maovu, basi seuze kuyatenda.

Na mabaya ni mabaya tu, ukiyafanya kwa dhahiri au kwa siri. Ndiyo maana yakakatazwa kwa zote hali zake mbili, ingawa kuyafanya dhahiri ni ubaya zaidi. Katika haki za kupelekea Serekali ya Kiislamu kumuua Muislamu ni:

(a) Kuacha dini yake akaingia dini ya Kikafiri. Watapelekwa wanavyuoni wapole mahodari wamfahamishe vilivyo kila mushkili alio nao. Akishika yale yale tu ayatakayo; hataki kufuata hoja wala dalili; basi Serikali itamwua.

(b) Kuacha kusali. Atapewa indhari (maonyo) kwanza mara mbili tatu. Akitosikia atauawa.

(c) Kuzini na hali ya kuwa amepata kuoa (au kuolewa) ijapokuwa sasa wajane. Ama ikiwa hajapata kuoa (au kuolewa) basi hauawi lakini atapigwa bakora 100 za kweli kweli mbele za watu.

*N.B.*—Ama ikiwa kwa kuendeana wanaume wenyewe kwa wenyewe, basi watauawa tu wakiwa walipata kuoa au hawajapata. Adabu yao ni kuuawa tu pale pale.

(d) Kuua mwenziwe kwa kusudi hata ikiwa mkewe aliyemfumania au huyo mwanamume aliyemfumani anaye. Basi mambo ya kuua wakati wa kufumaniana hayakubaliwi katika Sharia. Ima stahamili au mwache. Na kumwacha ndio bora kuliko kukaa naye. Na ukitaka kukaa naye unaweza. Hivi ndivyo yanavyosema madhehebu ya Kisuni. Ama kwa Kiibadhi anaachika pale pale ikiwa kweli ulimwona katika hali ya zina wala hakuhalalikii tena. Na vile vile mke akimfumania mume katika hali ya kufanya kitendo.

152. Kuna mawasii wengi wanaoachiwa mali ya mayatima; ima wakayaacha kuharibika au wakayaharibu wao au wakayachukua wao au wakayamegua kidogo au sana; basi adhabu kubwa inawangojea.

Wizi wa viapo umejaa katika nchi hizi. Wana vijinjia vingi vya kuwakhadaia hao wanunuzi au wauzaji. Basi wasione tamu hapa, Akhera adhabu kali inawangoja.

Ahadi za Mwenyezi Mungu ni kujiepusha na makatazo yote na kufanya kila analoliweza katika maamrisho yake.

Na zile ahadi za kheri wanazopeana watu wenyewe kwa wenyewe zinahisabika kuwa ni ahadi za Mwenyezi Mungu; lazima zitekelezwe khasa ahadi za kuozwa.

156. Msije (siku ya Kiama) mkasema: "Hakika Vitabu viliteremshwa juu ya makundi mawili ya kabla yetu (Mayahudi na Manasara), nasi tulikuwa hatuna habari ya yale waliyokuwa wakiyasoma "

أَن تَقُولُوٓا۟ إِنَّمَآ أُنزِلَ ٱلْكِتَٰبُ عَلَىٰ طَآئِفَتَيْنِ
مِن قَبْلِنَا وَإِن كُنَّا عَن دِرَاسَتِهِمْ لَغَٰفِلِينَ ١٥٦

157. Au mkasema: "Lau tungaliteremshiwa Kitabu bila shaka tungalikuwa waongofu zaidi kuliko wao." Basi (kwa kuletewa Mtume huyu na kuteremshwa Qurani) zimekufikieni hoja zilizo wazi kutoka kwa Mola wenu, na uwongofu na rehema (pia). Basi ni nani dhalimu mkubwa (anayedhulumu nafsi yake) kuliko yule anayezikadhibisha Aya za Mwenyezi Mungu na akajitenga nazo? Tutawalipa wale wanaojitenga na Aya zetu adhabu mbaya (kabisa) kwa sababu ya kule kujitenga kwao.

أَوْ تَقُولُوا۟ لَوْ أَنَّآ أُنزِلَ عَلَيْنَا ٱلْكِتَٰبُ لَكُنَّآ
أَهْدَىٰ مِنْهُمْ ۚ فَقَدْ جَآءَكُم بَيِّنَةٌ مِّن رَّبِّكُمْ
وَهُدًى وَرَحْمَةٌ ۚ فَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّن كَذَّبَ
بِـَٔايَٰتِ ٱللَّهِ وَصَدَفَ عَنْهَا ۗ سَنَجْزِى ٱلَّذِينَ
يَصْدِفُونَ عَنْ ءَايَٰتِنَا سُوٓءَ ٱلْعَذَابِ بِمَا كَانُوا۟
يَصْدِفُونَ ١٥٧

158. Wanangoja jengine ila wawafikie Malaika (kuwatoa roho) au iwafikie (adhabu kamili ya) Mola wako, au zifike baadhi ya Ishara za Mola wako (alizosema kuwa zitawafikia)? Siku zitakapofika baadhi ya Ishara za Mola wako, basi mtu (kafiri) haitamfaa imani yake, ambaye alikuwa hakuamini zamani, au (Mwislamu) hakuchuma kheri katika Uislamu wake. Sema: "Ngojeni, sisi pia tunangoja."

هَلْ يَنظُرُونَ إِلَّآ أَن تَأْتِيَهُمُ ٱلْمَلَٰٓئِكَةُ أَوْ يَأْتِىَ رَبُّكَ
أَوْ يَأْتِىَ بَعْضُ ءَايَٰتِ رَبِّكَ ۗ يَوْمَ يَأْتِى بَعْضُ
ءَايَٰتِ رَبِّكَ لَا يَنفَعُ نَفْسًا إِيمَٰنُهَا لَمْ تَكُنْ ءَامَنَتْ
مِن قَبْلُ أَوْ كَسَبَتْ فِىٓ إِيمَٰنِهَا خَيْرًا ۗ قُلِ
ٱنتَظِرُوٓا۟ إِنَّا مُنتَظِرُونَ ١٥٨

159. Hakika wale waliofarikisha dini yao na wakawa makundi makundi, huna ukhusiano nao wo

إِنَّ ٱلَّذِينَ فَرَّقُوا۟ دِينَهُمْ وَكَانُوا۟ شِيَعًا لَّسْتَ

153. Mtu akiacha kufuata aliyoyasema Mwenyezi Mungu na Mtumewe—hali yakuwa yako—akafuata ya watu wengine au akafuata anayoyataka mwenyewe; basi atakuwa kisha kuiacha njia ya Mwenyezi Mungu ya kumfikisha Peponi, kashika njia za shetani za kumpeleka Motoni.

*N.B.* Mara nyingi tunasema 'Haya ndiyo aliyoyasema Mwenyezi Mungu' au 'Haya ndiyo aliyoyasema Mtume.' Basi akichukia mtu kuyafuata atakuwa yumo katika khatari kubwa kabisa.

155. Inaonyesha kuwa wenye kufuata kitabu hiki watarehemeka tu duniani na Akhera. Na Waislamu walipokifuata kitabu hiki walirehemeka duniani na Akhera. Waliitawala nusu ya ulimwengu, wakastarehe wao na wakasitarehe waliowatawala, waliokuwa Waislamu na wasiokuwa Waislamu.

156-157. Wanaondoshewa udhuru, hawana la kusema.

Wametia upinzani wao tena wa kumpinga Mwenyezi Mungu katika hii Aya waliyofanya kuwa ni ya 157, wakasema kuwa *Ahlil kitabu* ni Mayahudi na wafuasi wa Zartashti *(Zoroaster)* yaani Maparisi; sio Manasara. Kila Mwislamu anajua na kuitakidi kuwa *Ahlul Kitab* ni Mayahudi (kwa ajili ya kitabu cha Taurati) na Manasara (kwa ajili ya kitabu cha Injili). Hakuna Mwislamu anayesema — ni Maparisi kwa ajili ya mtume wao Zoroaster na kitabu chao Zend-Avesta. Wapi Mwenyezi Mungu au Mtume wake alipomtaja mtume Zoroaster na kitabu chake, Zend-Avesta? Tazama ubaya wao katika kuwaharibu Waislamu wawe makafiri kama wao — kama anavyosema Mwenyezi Mungu katika Aya ya 89 ya *Suratun Nisaa* na Aya ya 2 ya *Suratul Mumtahina*. Natutahadhari na kukufurishwa nao. Hii ndiyo kazi iliyowaleta huku na kuletwa na hao wakubwa wao. Hawakuijia kazi nyingine ila hii ya kupoteza Waislamu.

Wakazidi kumpinga Mwenyezi Mungu wakasema:— "Wakristo hawakupewa Sheria ya peke yao . . ." Sasa vipi Mungu amesema katika Aya ya 47 ya *Suratul Maida* kuwa: "Na wahukumu wenye kupewa Injili (Manasara) kwa mujibu wa yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu ndani yake (hiyo Injili)"? Wao wanasema hamna sharia humo! Wamejiweka kumsuta Mwenyezi Mungu tu kwa kila anachokisema kisiwapendeze! Sio kazi ya Mwenyezi Mungu kuwaridhisha wao. Kazi yake ni kubainisha haki na kuondoa batili; kama anavyosema katika Aya ya 8 ya *Suratul Anfal* na chungu ya Aya nyinginezo. Wataendelea Waislamu wote kuitakidi—kama alivyosema Mwenyezi Mungu na Mtume wake—kuwa *Ahlul Kitab* ni Mayahudi na Manasara, si Mayahudi na Maparisi. Hatujui Maparisi nao wamewapa nini hata wakawatia katika *Uahlil Kitabu*. Mambo ya Nyumbani Kunga. Makuti ya Kumba. Lakini Mlango wa nyumba hiyo—waliyoijenga baina yao na Maparisi—ni wa Kumbesa; na nyumba

wote. Bila shaka shauri yao (ya kuwaadhibu) iko kwa Mwenyezi Mungu; kisha (hapo wakati wa kuwaadhibu) atawaambia yale waliyokuwa wakitenda.

مِنْهُمْ فِي شَيْءٍ ۚ إِنَّمَا أَمْرُهُمْ إِلَى اللَّهِ ثُمَّ يُنَبِّئُهُم بِمَا كَانُوا يَفْعَلُونَ ﴿١٥٩﴾

160. Afanyae kitendo kizuri, atalipwa mfano wake mara kumi. Na afanyae kitendo kibaya hatalipwa ila sawa nacho tu (basi, kwa rehema ya Mwenyezi Mungu). Nao (wote hao) hawatadhulumiwa.

مَن جَاءَ بِالْحَسَنَةِ فَلَهُ عَشْرُ أَمْثَالِهَا ۖ وَمَن جَاءَ بِالسَّيِّئَةِ فَلَا يُجْزَىٰ إِلَّا مِثْلَهَا وَهُمْ لَا يُظْلَمُونَ ﴿١٦٠﴾

---

yenyewe pia.

158. Uislamu sharti uuchumie mema. Uislamu mtupu hautoshi kukusaidia usiingie Motoni. Na Kafiri kusilimu kwake sharti asilimu katika hali ya uzima wake, siyo katika saa ya kukata roho.

Na Mwislamu mbaya kutubia kwake hakumfai vile vile saa ya kukata roho. Inataka atubie katika hali ya uzima wake ndipo Mwenyezi Mungu amkubalie. Sio kutubia saa anapoyaona mauti mbele ya macho yake. Hapo wataambiwa kama alivyoambiwa Firauni:- "Sasa (ndiyo unatubia)! Na kabla ya hapo ulikuwa ukiendelea tu kuasi na kufisidi. (Haifai kitu leo toba hiyo).

159. Waliofarikisha Dini yao — wakatia wasiyoambiwa au wakatoa waliyoambiwa kama Mayahudi walivyotia ushirikina wa kumshirikisha Mwenyezi Mungu na Uzayr na Manasara kumshirikisha Mwenyezi Mungu na Nabii Isa. Na dini nyingine za Mitume wa haki zilitiliwa ushirikina vile vile ulio wa ukafiri khasa kama huu wa Kiyahudi na Kinasara.

Ama Uislamu—*Al-hamdulillah*—ingawa umetiliwa ushirikina lakini si ule ushirikina khasa wa kuwatoa katika Uislamu. *Al-hamdulillah.*

Katika pepesi zilizotiwa ni hayo aliyoyataja Sheikh mkubwa kabisa wa Al Azhar na Mufattish wa ulamaa wote huko! Ameyataja haya katika sahifa 639 *Majallatul Azhar* ya mwezi wa Rajabu 1376 kwa kusema:— "Baadhi ya ulama wamelitoa katika maana yake tamko la *Wasila* lililotajwa katika Aya ya 35 ya *Suratil Maida*, wakalifanya kuwa miongoni mwa maana zake ni: (a) Kumwomba Mwenyezi Mungu kwa jaha ya wale mabwana wakubwa waliokufa au (b) Kuwaomba hao mabwana wakubwa waliokufa, wawaombee kwa Mwenyezi Mungu.

Hata ikawa inapita katika ndimi za wengi kutawasali (kuomba) kwa Bwana Fulani na Bwana Fulani . . . Bali imeingia katika nyoyo za baadhi yao kuwa mabwana walioko makaburini wana jaha na kupitisha wanayoyataka mbele ya Mwenyezi Mungu—wanasarifu mambo ya viumbe (wakaweka hili wakaondosha hili—ukiwaomba wanakufanyia wanavyotaka.)"

Akaendelea huyu Sheikh Abdul-Latifus Subky kusema: "Na wanapofuata fahamu hii wanaona kuwa kutawasali (kuomba) kwa walio makaburini ambao walikuwa wema katika uhai wao, (wanaona) ni jambo lililoamrishwa katika Qurani . . . wala sivyo kwani hali ya Qurani inakataza kabisa kwani Qurani imesimama juu ya msingi wa kumpwekesha Mwenyezi Mungu na washirika na (imesimama juu ya msingi) wa kuwaelekeza watu kwa Mola tu peke yake katika kila jambo — miongoni mwa mambo yao — likiwa kubwa au dogo (sio kuwaelekeza makaburini wala mizimuni wala . . ."

Akaendelea tena kusema: "Na haki isiyohitajia taklifu yo yote wala isiyokuwa na shaka yo yote ni hii: Kuwa Tawasuli huwa kwa amali njema zake mwenyewe mtu na huwa kwa dua njema anazoombewa na wenziwe walio hai; khasa wale wacha Mungu (sio kuombewa na walio maiti au kufanyiwa na hao maiti)."

Akaendelea zaidi kusema:- "Ama waliokufa kuwaombea walio hai halipatikani hilo wala halimkiniki wala hapana tamaa ya kupatikana wala hapana maana ya kutegemea hayo."

Wala haya hawasemi Ulamaa wa sasa tu wa Misri tu; bali ndivyo ilivyosemwa na kufanywa tangu hizo zama za mwanyo kabisa za Uislamu.

Mambo yalikorogeka kidogo zama za kati yakaendelea baadhi yake kudumu mpaka leo. Na jitihada za wanavyuoni wa sasa zote ni kutaka kuyarejesha mambo yawe kama yalivyokuwa katika zama za Masahaba na Matabiina. Na yatakuwa Inshaalah.

Imam Malik alikuwa akisema:- "Hautawatengeza watu wa mwisho wa uma huu ila ule ule mwendo uliowatengeneza watu wa mwanzo wao."

Na huku kuwataka watu wamwombe Mwenyezi Mungu tu pasi na kumwomba kwa wasila majina ya viumbe vyake, hata ulamaa wakubwa wa Hadhramoti wa zama hizo za mbele wamesema vivi hivi. Ameyataja haya Sheikh Abdulla bin Ahmad Ba Sawdan katika sahifa 124 ya sherehe yake juu ya Uradi wa Sayyidnal Haddad huu unaosomwa misikitini usiku.

Na vile vile inaingia katika Aya hii magombezi ya kufarikiana Waislamu wenyewe kwa wenyewe wakapigana

161. Sema: "Kwa hakika mimi Mola wangu ameniongoza katika njia iliyonyoka, (katika) dini iliyo sawa kabisa ambayo ndiyo dini ya Ibrahimu aliyekuwa mwongofu; wala (kabisa) hakuwa miongoni mwa washirikina."

قُلْ إِنَّنِي هَدَانِي رَبِّي إِلَىٰ صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ ۚ
دِينًا قِيَمًا مِلَّةَ إِبْرَاهِيمَ حَنِيفًا ۚ وَمَا كَانَ مِنَ
الْمُشْرِكِينَ ﴿١٦١﴾

162. Sema: "Hakika Sala yangu, na ibada zangu (zote nyingine) na uzima wangu, na kufa kwangu; (zote) ni kwa Mwenyezi Mungu. Mwumba wa walimwengu wote. ( Likinisibu jambo limenisibu kwa kutaka Mwenyezi Mungu si kwa kutaka viumbe vyake. Na yote ninayoyafanya nayafanya kwa ajili yake) "

قُلْ إِنَّ صَلَاتِي وَنُسُكِي وَمَحْيَايَ وَمَمَاتِي لِلَّهِ
رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١٦٢﴾

163. "Hana mshirika wake. Na haya ndiyo niliyoamrishwa, na mimi ni wa kwanza wa waliojisalimisha (kwa Mwenyezi Mungu)."

لَا شَرِيكَ لَهُ ۖ وَبِذَٰلِكَ أُمِرْتُ وَأَنَا أَوَّلُ
الْمُسْلِمِينَ ﴿١٦٣﴾

164. Sema: "Je, nishike mola mwingine asiyekuwa Mwenyezi Mungu, na hali Yeye (Mwenyezi Mungu) ndiye Mola wa kila kitu?" Wala nafsi yo yote haichumi (ubaya) ila ni juu yake; (hatalipwa kiumbe mwingine kwa ubaya wake). Wala mbebaji (mizigo yake ya dhambi) hatabeba mizigo ya mwingine (kumsaidia). Kisha marejeo yenu (nyote) ni kwa Mola wenu. Naye atakuambieni yale mliyokuwa mkihitalifiana.

قُلْ أَغَيْرَ اللَّهِ أَبْغِي رَبًّا وَهُوَ رَبُّ كُلِّ شَيْءٍ ۚ
وَلَا تَكْسِبُ كُلُّ نَفْسٍ إِلَّا عَلَيْهَا ۚ وَلَا تَزِرُ وَازِرَةٌ
وِزْرَ أُخْرَىٰ ۚ ثُمَّ إِلَىٰ رَبِّكُمْ مَرْجِعُكُمْ فَيُنَبِّئُكُمْ بِمَا
كُنْتُمْ فِيهِ تَخْتَلِفُونَ ﴿١٦٤﴾

165. Naye ndiye aliyekufanyeni washikaji wa mahala pa hao walioondoka katika hii ardhi (walioangamizwa huko zamani. Sasa muko nyinyi badala yao). Na amewanyanyua baadhi yenu juu ya wengine daraja kubwa kubwa (kwa utajiri, jaha, nasaba na mengineyo) ili akufanyieni mtihani kwa hayo aliyokupeni. (Aliyepewa hayo ayatumie kwa kuwasaidia wasiopewa). Hakika Mola wako ni Mwepesi wa kuadhibu, na hakika Yeye ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu (kwa wale wanaorejea kwake).

وَهُوَ الَّذِي جَعَلَكُمْ خَلَائِفَ الْأَرْضِ وَرَفَعَ بَعْضَكُمْ
فَوْقَ بَعْضٍ دَرَجَاتٍ لِيَبْلُوَكُمْ فِي مَا آتَاكُمْ ۗ إِنَّ
رَبَّكَ سَرِيعُ الْعِقَابِ وَإِنَّهُ لَغَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿١٦٥﴾

---

mapande kwa jina la (a) Madhehebu, la (b) Makabila, la (c) Nchi, la (d) miji na kama hivi.

Mambo mabaya kabisa hayo ya kufarikiana Waislamu wenyewe kwa wenyewe. Wanapiganishwa vichwa na wasiokuwa Waislamu, na wao wanakubali. Wamo katika khatari, na mateso makubwa yanawangoja. Wako mbali kabisa na Aliyosema Mwenyezi Mungu na Mtume.

160. Katika rehema za Mwenyezi Mungu juu ya viumbe Vyake ni kuwa atakapomlipa mtu Akhera kwa mema yake na mabaya yake atamlipa kwa namna hii: Jema moja kwa thawabu kumi (si thawabu moja). Lakini Baya moja kwa teso moja tu (si mateso kumi).

Na huku kulipa Jema moja kwa thawabu kumi ndio uchache wa kulipa kwa Jema moja; kwa kuwa Jema hilo hakulifanya kwa usafi sana. Ama akilifanya kwa usafi kabisa hupata moja kwa mia saba, bali na zaidi, kama alivyosema katika Aya ya 161 ya *Suratil Baqarah.*

161. Waarabu katika ibada zao hizo za ushirikina na upotofu wakisema wanafuata walivyofundishwa na Nabii Ibrahimu. Basi ndiyo wanavunjwa hivi: kuwa hayo ni uwongo. Nabii Ibrahimu hakuwa namna hivyo wanavyosema wao. Soma maelezo ya Aya ya 15 ya banii israel.

165. Kuonyesha kuwa utajiri na cheo na . . . sio alama ya kutukuzwa, na vile vile ufakiri na udhalilifu . . . si alama ya kutwezwa. Yote haya ni mitihani tu.

آياتها ٢٠٦ (٧) سُورَةُ الأَعْرَافِ مَكِّيَّةٌ (٣٩) رُكُوعَاتُهَا ٢٤

*Ina Aya 206* **SURAT AL - AARAF** *Ina Makara 24*

*(Imeteremka Makka)*

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

1. Alif Lam Mym Sad.

المص ①

2. (Hii Qurani ni) Kitabu (kitukufu) kilichoteremshwa kwako. Basi isiwe dhiki kifuani kwako kwa ajili yake (kitabu hicho). (Umeteremshiwa) ili upate kuonya kwacho, na kiwe ni mauidha kwa walioamini.

كِتَابٌ أُنزِلَ إِلَيْكَ فَلَا يَكُن فِي صَدْرِكَ حَرَجٌ
مِّنْهُ لِتُنذِرَ بِهِ وَذِكْرَىٰ لِلْمُؤْمِنِينَ ②

3. Fuateni mliyoteremshiwa kutoka kwa Mola wenu, wala msifuate (hao mnaowaitakidi kuwa) walinzi badala yake. Ni machache mnayoyakumbuka.

اتَّبِعُوا مَا أُنزِلَ إِلَيْكُم مِّن رَّبِّكُمْ وَلَا تَتَّبِعُوا مِن
دُونِهِ أَوْلِيَاءَ ۗ قَلِيلًا مَّا تَذَكَّرُونَ ③

4. Na miji mingapi tuliiangamiza; na iliifikia adhabu Yetu usiku au katika wakati wa adhuhuri walipokuwa wamelala (kupumzika).

وَكَم مِّن قَرْيَةٍ أَهْلَكْنَاهَا فَجَاءَهَا بَأْسُنَا بَيَاتًا أَوْ هُمْ
قَائِلُونَ ④

5. Basi hakikuwa kilio chao ilipowafikia adhabu Yetu isipokuwa kusema: "Bila shaka sisi tulikuwa madhalimu (na sasa tunarejea." Lakini hayakuwafaa kitu hayo).

فَمَا كَانَ دَعْوَاهُمْ إِذْ جَاءَهُم بَأْسُنَا إِلَّا أَن قَالُوا
إِنَّا كُنَّا ظَالِمِينَ ⑤

6. Na kwa yakini tutawauliza wale waliopelekewa (Mitume), na pia tutawauliza (Mitume) waliopelekwa

فَلَنَسْأَلَنَّ الَّذِينَ أُرْسِلَ إِلَيْهِمْ وَلَنَسْأَلَنَّ الْمُرْسَلِينَ ⑥

7. Tena tutawaambia kwa ujuzi (uliyo kamili kila walilolitenda). Wala hatukuwa mbali (nao walipokuwa wakiyafanya).

فَلَنَقُصَّنَّ عَلَيْهِم بِعِلْمٍ ۖ وَمَا كُنَّا غَائِبِينَ ⑦

8. Na siku hiyo kipimo kitakuwa sawa (kabisa cha kulipwa kila mtu amali zake). Basi watakaokuwa na uzani mzito, hao ndio watakaofaulu.

وَالْوَزْنُ يَوْمَئِذٍ الْحَقُّ ۚ فَمَن ثَقُلَتْ مَوَازِينُهُ
فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ ⑧

9. Na watakaokuwa na uzani khafifu, basi hao ndio waliozitia hasarani nafsi zao kwa sababu ya kuzifanyia ujeuri Aya zetu.

وَمَنْ خَفَّتْ مَوَازِينُهُ فَأُولَٰئِكَ الَّذِينَ خَسِرُوا
أَنفُسَهُم بِمَا كَانُوا بِآيَاتِنَا يَظْلِمُونَ ⑨

---

2. Hapa anaambiwa Mtume asiogope kutangaza aliyokuja nayo, asiwajali wapingaji hata wakiwa wengi vipi. Basi na kila mwanachuoni anamrishwa vivi hivi. Apasue tu asijali. Apige Hodi, apige Bisumila, asonge mbele kutangaza haki bila ya kumwogopa yo yote. Piga Hodi usonge mbele:

Hodi hodi nasumiza — Waoga kando
Naonyesha maadui — Vikubwa vihendo
Siogopi wao moto — Mimi ni nyundo

8. Cha kufuzia Akhera ni amali njema unazozichuma huku duniani. Basi tujitahidi kuongeza amali njema

10. Na hakika tumekumakinisheni (tumekukalisheni) katika ardhi na tumekuwekeeni humo (vitu vyote) vinavyohitajia maisha yenu. Ni shukurani chache tu mnayoshukuru (bali hamshukuru cho chote).

وَلَقَدْ مَكَّنَّٰكُمْ فِى ٱلْأَرْضِ وَجَعَلْنَا لَكُمْ فِيهَا مَعَٰيِشَ ۗ قَلِيلًا مَّا تَشْكُرُونَ ﴿١٠﴾

11. Na hakika tulikuumbeni, kisha tukakutieni sura, kisha tukawaambia Malaika: "Msujudieni Adamu." Basi wakasujudu isipokuwa Ibilisi hakuwa miongoni mwa waliosujudu.

وَلَقَدْ خَلَقْنَٰكُمْ ثُمَّ صَوَّرْنَٰكُمْ ثُمَّ قُلْنَا لِلْمَلَٰٓئِكَةِ ٱسْجُدُوا۟ لِءَادَمَ فَسَجَدُوٓا۟ إِلَّآ إِبْلِيسَ لَمْ يَكُن مِّنَ ٱلسَّٰجِدِينَ ﴿١١﴾

12. (Mwenyezi Mungu) akasema: "Nini kilichokuzuia kumsujudia nilipokuamrisha?" Akasema: "Mimi ni bora kuliko yeye. (Mimi) umeniumba kwa moto, naye umemumba kwa udongo."

قَالَ مَا مَنَعَكَ أَلَّا تَسْجُدَ إِذْ أَمَرْتُكَ ۖ قَالَ أَنَا۠ خَيْرٌ مِّنْهُ خَلَقْتَنِى مِن نَّارٍ وَخَلَقْتَهُۥ مِن طِينٍ ﴿١٢﴾

13. Akasema (Mwenyezi Mungu): "Basi shuka huko, haikufalii kufanya kiburi humo. (Haya) toka; hakika wewe u miongoni mwa wadhalilifu."

قَالَ فَٱهْبِطْ مِنْهَا فَمَا يَكُونُ لَكَ أَن تَتَكَبَّرَ فِيهَا فَٱخْرُجْ إِنَّكَ مِنَ ٱلصَّٰغِرِينَ ﴿١٣﴾

14. Akasema: "Nipe muda (nisife) mpaka siku watakapofufuliwa (viumbe)."

قَالَ أَنظِرْنِىٓ إِلَىٰ يَوْمِ يُبْعَثُونَ ﴿١٤﴾

15. Akasema (Mwenyezi Mungu): "Utakuwa miongoni mwa waliopewa muda, (lakini si mpaka wakati huo)."

قَالَ إِنَّكَ مِنَ ٱلْمُنظَرِينَ ﴿١٥﴾

---

11. Imesemwa hapa: "Tulikuumbeni kisha tukakutieni sura;" na hali ya kuwa bado ilikuwa hawajaumbwa Binaadamu. Lakini kwa kuwa amekwishakuumbwa mzee wao—naye ni Nabii Adamu—basi inakuwa ndiyo kama wamekwishakuumbwa.

Na sijida hiyo ilikuwa ya taadhima si ya ibada.

Katika Aya waliyoita ya 12 wametia upotezi wao ule ule wa kusema kuwa Nabii Adamu hakuwa Peponi mbinguni; na hali ya kuwa Mwenyezi Mungu amewaambia—kama ilivyo katika Aya ya 36 na ya 38 ya *Suratul Baqarah* na Aya ya 23 ya *Suratul Aaraf* — "Teremkeni huko na mtapata maisha yenu katika ardhi." Hatutaacha sisi maneno ya Mwenyezi Mungu tukafuata maelezo (Mapotezo) yao. Na habari hii tumekwisha kuivunja katika kuvunja maelezo ya Aya ya 36 ya *Suratul Baqarah.*

Wakazidisha hapa uwongo wao wakasema: "Hadithi pia inaeleza kuwa Iraq Arab (Mespotamia) ambayo ni ardhi yenye Furata na Tigris ndipo mahali zilipopatikana habari za Adamu." Tazama ukafiri wao wa kumsingizia uwongo Mtume. Iko mahala gani Hadithi hiyo katika vitabu Sahihi vya Hadithi za Mtume? Majasuri kweli kweli. Mtume amesema "Atakayenisingizia uwongo ataingia Motoni" tu, na wao hawajali hawabali, wanamsingizia uwongo Mtume na kumsusuwika Mwenyezi Mungu kinaga ubaga.

Tazama wanavyojipinga wenyewe. Hapa sasa wanakataa wanasema kuwa Iblisi hakumsemeza Nabii Adamu kwa sababu Iblisi "ni katika Majini (yaani viumbe visivyoonekana)." Mara moja kiasi cha kufika Sura hii tu iliyo ubavuni mwa *Suratul An-am* wamesahau kuwa wamesema katika Aya walizozifanya za 113 na 129 na 131 za *Suratul An-am* kuwa Majini ndio Binaadamu si viumbe vyengine. Walivyokuwa sasa wanataka kumpinga Mungu tena, wamemsuta wanasema Iblisi hakusemeza Nabii Adamu kwani Iblisi ni katika Majini, viumbe visivyoonekana. Shabash! Wasiwe na kazi ila kumsuta Mwenyezi Mungu na kumwona mwongo. Waongo wao. Ulimwengu mzima Unawasuta na kope zao Zinawasusuwika! Ati asiyeonekana hasikilizani! Wanaosema katika Maredio—kabla ya kuvumbuliwa Television—walikuwa wakionekana au wakisikilizana tu? Hizaya yao — kichwa chini miguu juu. Maadamu Mwenyezi Mungu, katika Qurani nzima, ametwambia kuwa Iblisi alimsemeza Nabii Adamu na mkewe: *"Waqaala Maa Nahaakumaa"* na amewaapia *"Waqaasamahumaa,"* basi hatutawasikiliza wao tukamkadhibisha Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu anasema katika Aya ya 140 ya *Suratul Baqarah "Aantum A'alamu Amil Laahu"* (nyinyi ndio munaojua—au mnaojua zaidi—au Mwenyezi Mungu)? Hapana shaka kuwa anayejua ni Mwenyezi Mungu.

16. Akasema: "Kwa kuwa umenihukumia upotofu (upotevu) basi nitawakalia (waja Wako) katika njia Yako iliyonyoka (ili niwapoteze)"

قَالَ فَبِمَآ أَغْوَيْتَنِى لَأَقْعُدَنَّ لَهُمْ صِرَٰطَكَ ٱلْمُسْتَقِيمَ ﴿١٦﴾

17. "Kisha nitawafikia kwa mbele yao na nyuma yao na kuumeni (kuliani) kwao na kushotoni kwao; wengi katika wao hutawakuta (hutawaona) ni wenye kukushukuru."

ثُمَّ لَءَاتِيَنَّهُم مِّنۢ بَيْنِ أَيْدِيهِمْ وَمِنْ خَلْفِهِمْ وَعَنْ أَيْمَٰنِهِمْ وَعَن شَمَآئِلِهِمْ ۖ وَلَا تَجِدُ أَكْثَرَهُمْ شَٰكِرِينَ ﴿١٧﴾

18. Akasema (Mwenyezi Mungu): "Toka humo, hali ya kuwa ni mwenye kudharauliwa na mwenye kufukuzwa. Atakayekufuata miongoni mwao, (nitamtia Motoni) niijaze Jahanamu kwa nyinyi nyote."

قَالَ ٱخْرُجْ مِنْهَا مَذْءُومًا مَّدْحُورًا ۖ لَّمَن تَبِعَكَ مِنْهُمْ لَأَمْلَأَنَّ جَهَنَّمَ مِنكُمْ أَجْمَعِينَ ﴿١٨﴾

19. (Kisha Mwenyezi Mungu akasema kumwambia Nabii Adamu): "Na wewe Adamu! Kaa Peponi pamoja na mkeo, na kuleni mnapopenda, lakini msiukaribie mti huu msije kuwa miongoni mwa waliodhulumu (nafsi zao)."

وَيَٰٓـَٔادَمُ ٱسْكُنْ أَنتَ وَزَوْجُكَ ٱلْجَنَّةَ فَكُلَا مِنْ حَيْثُ شِئْتُمَا وَلَا تَقْرَبَا هَٰذِهِ ٱلشَّجَرَةَ فَتَكُونَا مِنَ ٱلظَّٰلِمِينَ ﴿١٩﴾

20. Basi Shetani; (naye ni yule Iblisi), aliwatia wasiwasi ili kuwadhihirishia aibu zao walizofichiwa, na akasema: "Mola wenu hakukukatazeni mti huu ila (kwa sababu hii:) msije kuwa Malaika au kuwa miongoni mwa wakao milele (wasife)."

فَوَسْوَسَ لَهُمَا ٱلشَّيْطَٰنُ لِيُبْدِىَ لَهُمَا مَا وُۥرِىَ عَنْهُمَا مِن سَوْءَٰتِهِمَا وَقَالَ مَا نَهَىٰكُمَا رَبُّكُمَا عَنْ هَٰذِهِ ٱلشَّجَرَةِ إِلَّآ أَن تَكُونَا مَلَكَيْنِ أَوْ تَكُونَا مِنَ ٱلْخَٰلِدِينَ ﴿٢٠﴾

21. Naye akawaapia (kuwaambia): "Kwa yakini mimi ni mmoja wa watowao shauri njema kwenu"

وَقَاسَمَهُمَآ إِنِّى لَكُمَا لَمِنَ ٱلنَّٰصِحِينَ ﴿٢١﴾

22. Basi akawateka (wote wawili) kwa khadaa (yake). Na walipouonja mti ule, aibu zao ziliwadhihirikia na wakaingia kujibandika majani ya (miti ya huko) Peponi. Na Mola wao akaweta (akawaambia) "Je, sikukukatazeni mti huu na kukwambieni ya kwamba Shetani ni adui yenu aliye dhahiri?"

فَدَلَّىٰهُمَا بِغُرُورٍ ۚ فَلَمَّا ذَاقَا ٱلشَّجَرَةَ بَدَتْ لَهُمَا سَوْءَٰتُهُمَا وَطَفِقَا يَخْصِفَانِ عَلَيْهِمَا مِن وَرَقِ ٱلْجَنَّةِ ۖ وَنَادَىٰهُمَا رَبُّهُمَآ أَلَمْ أَنْهَكُمَا عَن تِلْكُمَا ٱلشَّجَرَةِ وَأَقُل لَّكُمَآ إِنَّ ٱلشَّيْطَٰنَ لَكُمَا عَدُوٌّ مُّبِينٌ ﴿٢٢﴾

---

20. Makadiyani walipofika hii Aya walioifanya kuwa ni 21 uliwajia ushetani wao wa kugeuza maneno ya Mwenyezi Mungu ambao haukuwapitia walipolieleza tamko hili katika Aya ya 35 ya *Suratul Baqarah*. Huko walisema *"Shajarah* = ugomvi," tukawarejesha huko. Hapa wanasema sasa "Na Adamu anasemwa kuwa alikatazwa kuusogelea 'mti' ambao hakika yake ni ukoo au kabila aliloambiwa ajiweke mbali nalo . . ." Mungu kasema mti, wao wanasema ukoo au kabila! Mwenyezi Mungu hajui tamko la ukoo au la kabila? Au ukoo na kabila huliwa? Kwani Mwenyezi Mungu amesema: *"Faakalaa Minha"* (Adamu na mkewe wakala katika mti huo). Basi ukoo na kabila huliwa, zikatiwa kinywani zikatafunwa? Au kabila gani hiyo au hizo, au ukoo gani huo au hizo, zilizokuwako wakati huo, na hali ya kuwa yeye ndiye mzazi wa mwanzo wa Binaadamu wote? Lakini tumeona walivyomkanusha Mwenyezi Mungu wakasema kuwa Nabii Adamu siye Binaadamu wa mwanzo. Watajitia kichaa wenyewe hawatatutia sisi Waislamu.

22. Na wameipinga tena Qurani katika Aya hii waliyoifanya kuwa ni 23 wanasema: "Adamu na mkewe kudhihirikiwa na aibu zao kunakutajwa na Aya hii sio muradi wake kwamba walibaki utupu . . . bali ni kwamba baadhi ya upungufu na udhaifu wao walikuwa hawaujui . . ." Enyi wapotezi! Udhaifu na Upungufu hufunikwa kwa majani? Na Mwenyezi Mungu kasema—kama ilivyo katika hii Aya ya 22 ya *Suratul Aaraf* na katika Aya ya 121 ya *Taha*—kuwa "Wakaingia kujibandika majani ya (miti ya huko Peponi)." Hatutaacha kumsikiliza Mwenyezi Mungu tukawasikiliza wao.

23. Wakasema: "Mola wetu! Tumedhulumu nafsi zetu; na kama hutusamehe na kuturehemu, bila shaka tutakuwa miongoni mwa wenye khasara (kubwa, kabisa)."

قَالَا رَبَّنَا ظَلَمْنَا أَنفُسَنَا وَإِن لَّمْ تَغْفِرْ لَنَا
وَتَرْحَمْنَا لَنَكُونَنَّ مِنَ الْخَاسِرِينَ ﴿٢٣﴾

24. Akasema (Mwenyezi Mungu): "Shukeni (katika ardhi), nyinyi kwa nyinyi ni maadui. Na makao yenu yatakuwa katika ardhi, na starehe yenu (pia); mpaka muda (niutakao mimi Mwenyewe Mwenyezi Mungu)."

قَالَ اهْبِطُوا بَعْضُكُمْ لِبَعْضٍ عَدُوٌّ ۖ وَلَكُمْ فِي
الْأَرْضِ مُسْتَقَرٌّ وَمَتَاعٌ إِلَىٰ حِينٍ ﴿٢٤﴾

25. Akasema (Mwenyezi Mungu): "Mtaishi humo na mtafia humo, na mtatolewa humo" (mtafufuliwa kwenda Akhera kulipwa).

قَالَ فِيهَا تَحْيَوْنَ وَفِيهَا تَمُوتُونَ وَمِنْهَا
تُخْرَجُونَ ﴿٢٥﴾

26. (Anasema Mwenyezi Mungu kuwaambia wanaadamu wote tangu hao wa zamani huko): "Enyi wanaadamu! Hakika tumekuteremshieni nguo zifichazo tupu zenu na nguo za pambo; na nguo za

يَا بَنِي آدَمَ قَدْ أَنزَلْنَا عَلَيْكُمْ لِبَاسًا يُوَارِي
سَوْآتِكُمْ وَرِيشًا ۖ وَلِبَاسُ التَّقْوَىٰ ذَٰلِكَ خَيْرٌ ۚ ذَٰلِكَ

---

Lakini hawakuliwacha pia tamko la "*Waraqa*" (majani) alilolitumia Mwenyezi Mungu, wakasema maana ya *Waraqa* = vijana wadogo: "Shetani alifanikiwa kuingiza mfaraka katika wafuasi wa Adamu na waliokuwa na imani dhaifu miongoni mwao wakatoka; Nabii Adamu akaanza kukusanya *auraaq* (majani) ya bustani yaani vijana katika wafuasi wake (Akhrab, Lane Lisan) na akaanza kuwaunganisha na kuwatia umoja watu wake kwa msaada wa vijana hao."

Watu wake gani hao waliomfariki Adamu hata akataka msaada kwa vijana? Watu hao na vijana hao walitoka wapi? Na hali ya kuwa Nabii Adamu alikuwa yeye na mkewe na watoto wao tu—kisha wakawa wanakuja wajukuu kidogo kidogo na vitukuu. Enyi watu nyi! Mnapindukia mipaka katika kufanya kazi yenu hii ya kuikoroga dini hata inakuwa hata mjinga anaweza kukutambuweni. Shetani wenu sasa anakuondoleeni sitara yenu. Na uwongo kabisa hakusema haya huyo Lane wala mwenye Akrab wala mwenye Lisan. Kwanza hivi si vitabu vya tafsiri ya Qurani wala si vitabu vya kufasiri maneno magumu yaliyomo katika Qurani. Kwa nini hawatutajii kimoja katika vilevitabu vya Tafsiri walivyovitaja mwanzo wa tafsiri yao, wala kimoja katika vile vitabu vya kufasiri maneno ya Qurani walivyovitaja mwanzo wa tafsiri yao? Wanajua yakini kuwa hamna humo tafsiri ya ukafiri huo. Cheybar! Endeleeni tu katika kuwapoteza Waislamu.

Mja aliyeongoka
Mola akamwongowa
Haramu! Ujapotaka
Katika haki kumtowa
Utajikusa mashaka
Katu hutampotowa
Hidaya ndake Moliwa
Hapotoki kwa Shetani.

24. Shetani adui wa Binaadamu, na Binaadamu adui wa Shetani. Na Binaadamu ni adui wa Binaadamu wenziwao. Na mashetani nao pia. Muradi mchafukoge; na starehe ya kweli iwe Akhera.

Wanaona katika Aya hii waliyoifanya ya 25 kuwa Mwenyezi Mungu anamwambia Nabii Adamu na wenziwe: "*Walakum Fil Ardhi Mustaqarr*" [Na mtapata (sasa) makazi yenu katika ardhi] au [makao yenu (sasa) yatakuwa katika ardhi = badala ya Peponi] Wanamwona Mwenyezi Mungu anavyosema hivi katika nafsi ya hii Aya; na wao wamesema hivi: "Aya hii inaonyesha ya kuwa Adamu aliamrishwa kuhama nchi aliyozaliwa kwa sababu kulitokea uadui baina ya watu wake . . ." Mnaona upinduzi wao ulivyo katika kupindua maneno ya Mwenyezi Mungu! Na hapa ukafiri mwingine wao unatokeya na unatokeza. Wanasema kuwa Nabii Adamu amezaliwa: (nchi *aliyozaliwa*)! Mwenyezi Mungu anasema Nabii Adamu hana baba wala mama "*Khalaqahuu Min Turaabin*" (Amemwumba kwa mchanga tu); "*Thumma Qaala Lahuu Kun*" (Kisha akamwambia kuwa mtu); "*Fayakuun*" (Akawa mtu). Wao wanayakataa haya, na hali ya kuwa Mwenyezi Mungu ameyasema katika Aya ya 59 ya *Surat Aali Imrani* na ndiyo Qurani yote nzima inavyoonyesha vivi hivi. Wao wanamkanusha Mwenyezi Mungu wanasema: Nabii Adamu amezaliwa, hakuumbwa kwa muujiza wa qudra ya Mwenyezi Mungu. Wao maisha wanaikatalia qudra ya Mwenyezi Mungu kuweza kufanya miujiza.

25. Katika Aya hii walioifanya ni ya 26 wameyapachikia maelezo yao ili kukataa kuwa Nabii Isa amekwenda mbinguni.

مِنْ آيَاتِ اللَّهِ لَعَلَّهُمْ يَذَّكَّرُونَ ﴿٢٦﴾

utawa (yaani kucha Mungu) ndizo bora.[26] Hayo ni katika Ishara za (neema za) Mwenyezi Mungu ili wapate kukumbuka.

يَا بَنِي آدَمَ لَا يَفْتِنَنَّكُمُ الشَّيْطَانُ كَمَا أَخْرَجَ أَبَوَيْكُمْ
مِنَ الْجَنَّةِ يَنْزِعُ عَنْهُمَا لِبَاسَهُمَا لِيُرِيَهُمَا سَوْآتِهِمَا ۚ
إِنَّهُ يَرَاكُمْ هُوَ وَقَبِيلُهُ مِنْ حَيْثُ لَا تَرَوْنَهُمْ ۗ
إِنَّا جَعَلْنَا الشَّيَاطِينَ أَوْلِيَاءَ لِلَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿٢٧﴾

27. "Enyi wanaadamu! Shetani (Iblisi) asikutieni katika matata, kama alivyowatoa wazee wenu katika Pepo; akawavua nguo zao ili kuwaonyesha tupu zao. Hakika yeye pamoja na kabila yake wanakuoneni, na hali ya kuwa hamwaoni." Bila shaka sisi tumewajaalia mashetani kuwa marafiki wa wale wasioamini.

وَإِذَا فَعَلُوا فَاحِشَةً قَالُوا وَجَدْنَا عَلَيْهَا آبَاءَنَا
وَاللَّهُ أَمَرَنَا بِهَا ۗ قُلْ إِنَّ اللَّهَ لَا يَأْمُرُ
بِالْفَحْشَاءِ ۖ أَتَقُولُونَ عَلَى اللَّهِ مَا لَا تَعْلَمُونَ ﴿٢٨﴾

28. Na (makafiri) wanapofanya mambo machafu husema: "Tumewakuta nayo baba zetu na (pia) Mwenyezi Mungu ametuamrisha hayo." Sema: "Mwenyezi Mungu haamrishi mambo mabaya. Mnasema juu ya Mwenyezi Mungu msiyoyajua?"

قُلْ أَمَرَ رَبِّي بِالْقِسْطِ ۖ وَأَقِيمُوا وُجُوهَكُمْ عِنْدَ
كُلِّ مَسْجِدٍ وَادْعُوهُ مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ ۚ
كَمَا بَدَأَكُمْ تَعُودُونَ ﴿٢٩﴾

29. Sema: "Mola wangu ameamrisha uadilifu, na (ameniambia nikuambieni) elekezeni nyuso zenu (kwake) wakati wa kila Sala na mwabuduni yeye tu kwa utii khalisi. Kama alivyokuumbeni kwanza (mkitoka kwake) ndivyo mtavyorudi (kwake)."

فَرِيقًا هَدَىٰ وَفَرِيقًا حَقَّ عَلَيْهِمُ الضَّلَالَةُ ۗ إِنَّهُمُ
اتَّخَذُوا الشَّيَاطِينَ أَوْلِيَاءَ مِنْ دُونِ اللَّهِ
وَيَحْسَبُونَ أَنَّهُمْ مُهْتَدُونَ ﴿٣٠﴾

30. "(Hali ya kuwa) ameliongoa kundi moja; na kundi jingine limethubutikiwa na upotofu (upotevu)." Kwa hakika waliwafanya mashetani kuwa walinzi (wao au waola wao khasa) badala ya Mwenyezi Mungu, na wanadhani ya kuwa wao wameongoka.

يَا بَنِي آدَمَ خُذُوا زِينَتَكُمْ عِنْدَ كُلِّ مَسْجِدٍ وَكُلُوا

31. "Enyi wanaadamu! Chukueni mapambo yenu wakati wa kila Sala; na kuleni (vizuri) na kunyweni (vizuri). Lakini msipite kiasi tu. Hakika

---

26. Mwenyezi Mungu anatwambia tuyatumie mavazi aliyotuumbia ya kupamba miili yetu. Lakini anatuamrisha zaidi tutumie mavazi ya kupamba nafsi zetu na nyoyo zetu na roho zetu. Nguo za utawa (Vazi la kucha Mungu). Na mcha Mungu ni yule anayejiepusha na yote aliyoyakataza Mwenyezi Mungu na akafanya—kama anavyoweza—yale aliyoyaamrisha Mwenyezi Mungu. Wala si kazi ngumu sana kufanya haya.

27. Wanaomwamini Mwenyezi Mungu kweli kweli wakafuata tuliyoyataja katika Aya ya 26. Shetani hawezi kuwachezea.

28. Haya ni kama yale tuliyoyataja katika Aya ya 125 ya *Suratul An-am.*

30. Basi hivi tunaambiwa Waislamu tusitafute walinzi wengine. Mlinzi wa kweli ni Mwenyezi Mungu tu. Siyo kupewa mtoto pepo wa Bibi yake au wa yaya au wa mama au wa nyumba au . . . amlinde; khalafu pepo atapewa tunza yake. Au kupewa kaburi la Sharifu Musa limlinde au kaburi la mwinginewe. Huo ni ushirikina si Uislamu ingawa baadhi ya Waislamu wanafanya. Wanaweka nadhiri kuwa mtoto huyo atakuja nyolewa Sharifu Musa au atasomewa hapo Maulidi yake ya Jando au Akikua hata akaoa basi 'Bwana Sharifu Utapata Haluwa yako.' Yote hayo sivyo ulivyosema Uislamu. Mlinzi ni Mwenyezi Mungu; hakuna mlinzi mwengine.

Bali hata vihirizi Mtume kavikataza, basi seuze kufungwa vitambara vya Mvuje au vigwe. Natuache haya; tumtegemee Mwenyezi Mungu tu basi. Kila mwanachuoni aliyesoma anaweza kukuonyesha hadithi za mtume zilizokataza haya; wala hawezi kuvumbua zilizokubalisha.

31. Wanapewa ruhusa Waislamu wale vizuri, wanywe vizuri, wavae vizuri, wakae pazuri . . . Na wende misikitini na nguo nzuri.

Yeye (Mwenyezi Mungu) hawapendi wapitao kiasi (wapindukiyao mipaka).

وَاشْرَبُوا وَلَا تُسْرِفُوا ۚ إِنَّهُ لَا يُحِبُّ الْمُسْرِفِينَ ﴿٣١﴾

32. Sema: "Ni nani aliyeharimisha mapambo ya Mwenyezi Mungu ambayo amewatolea waja wake. Na (nani aliyeharimisha) vitu vizuri katika vyakula?" Sema: "Vitu hivyo vimewahalalikia Waislamu (hapa) katika maisha ya dunia; (na) vitakuwa vyao peke yao siku ya Kiyama." Namna hivi tunazieleza Aya kwa watu wajuao.

قُلْ مَنْ حَرَّمَ زِينَةَ اللَّهِ الَّتِي أَخْرَجَ لِعِبَادِهِ
وَالطَّيِّبَاتِ مِنَ الرِّزْقِ ۚ قُلْ هِيَ لِلَّذِينَ آمَنُوا
فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا خَالِصَةً يَوْمَ الْقِيَامَةِ ۗ كَذَٰلِكَ
نُفَصِّلُ الْآيَاتِ لِقَوْمٍ يَعْلَمُونَ ﴿٣٢﴾

33. Sema (uwaambie): "Mola wangu ameharimisha (Haya: Ameharimisha) mambo machafu, yaliyodhihirika na yaliyofichika, na dhambi na kutoka katika taa (ya wakubwa) pasipo haki, na kumshirikisha Mwenyezi Mungu na ambacho hakukiteremshia dalili (ya kusema kishirikishwe naye) na (ameharimisha) kusema juu ya Mwenyezi Mungu msiyoyajua."

قُلْ إِنَّمَا حَرَّمَ رَبِّيَ الْفَوَاحِشَ مَا ظَهَرَ مِنْهَا
وَمَا بَطَنَ وَالْإِثْمَ وَالْبَغْيَ بِغَيْرِ الْحَقِّ وَأَنْ تُشْرِكُوا
بِاللَّهِ مَا لَمْ يُنَزِّلْ بِهِ سُلْطَانًا وَأَنْ تَقُولُوا عَلَى
اللَّهِ مَا لَا تَعْلَمُونَ ﴿٣٣﴾

34. Na kila watu wana muda wao (wa kuondoka ulimwenguni). Utakapowafikia muda wao huo, hawatakawia (hata) saa moja wala hawatatangulia (kabla haujafika).

وَلِكُلِّ أُمَّةٍ أَجَلٌ ۖ فَإِذَا جَاءَ أَجَلُهُمْ لَا
يَسْتَأْخِرُونَ سَاعَةً ۖ وَلَا يَسْتَقْدِمُونَ ﴿٣٤﴾

35. Enyi wanaadamu! Watakapokufikieni Mitume miongoni mwenu (wanaadamu), wanakuelezeni Aya zangu. Basi watakaojikinga na wanayokatazwa, na wakafanya mema, basi haitakuwa khofu juu yao, wala hawatahuzunika.

يَا بَنِي آدَمَ إِمَّا يَأْتِيَنَّكُمْ رُسُلٌ مِنْكُمْ يَقُصُّونَ
عَلَيْكُمْ آيَاتِي ۙ فَمَنِ اتَّقَىٰ وَأَصْلَحَ فَلَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ
وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿٣٥﴾

---

Linalokatazwa ni Israfu tu (kutumia kwa fujo).

Na hili ndilo linalofanywa na watu walio wafujaji tangu zamani na walio mabakhili. Wote hao hutokewa na Vipindi vya kuwapelekea kufanya Israfu. Wakizaa watafanya hayo makaramu ya Israfu. Wakitahiri watafanya hayo. Wakioza watafanya. Wakifiwa pia watafanya hayo.

Kama tulivyosema kuwa wanafanya haya walio watumizi tangu zamani na walio mabakhili pia, na wanaojiweza na stiri hali na walio masikini. Wote hali moja. Cha mitungini kitatoka tu kwa mambo yale na cha makashani; khasa ikiwa kwa ajili ya matanga! Kwani wanaitakidi kuwa ni dini kufanya hayo ya matanga, na hali ya kuwa hata moja katika hayo si la dini.

32. Kulikuwako watu wengine waliokuwa wakiitakidi kuwa kucha Mungu ni kujitia taabuni na kuvaa mararuraru. Na mpaka leo wako watu namna hao; basi Mwenyezi Mungu akateremsha Aya hizi.

33. Mabaya ni mabaya tu kuyafanya. Ukiyafanya kwa jahara hivi bila ya kujali na ukiyafanya kwa kificho pia. Yote ni mabaya; yatakudhuru tu duniani na Akhera. Ila yale yanayofanywa kwa jahara huzidi tu ubaya wake; lakini yote ni mabaya.

35. Amri hii ya 35 ni kama amri zile zote zilizotangulia tangu Aya ya 26 ya Sura hii. Ni amri walizopewa kila uma uliokuja, tangu Nabii Adamu mpaka kuja huyu Mtume wa mwisho Sayyidna Muhammad. (s.a.w.).

Si kuwa amri hii inakhusu uma huu wa Nabii Muhammad na kuwa inaonyesha kuwa baada ya Nabii Muhammad atakuja Mtume mwengine, naye ni huyo Kadiyani wao kama wanavyodai hao Makadiyani wapotoaji wa tafsiri ya Qurani kusudi ili kuwapoteza Waislamu.

Uwongo kabisa hivyo wasemavyo wao, kama Aya zilizotangulia zote zinavyoyowasuta. Lakini wana nyuso za watu wa mahala Fulani ambao watajitahidi Siku ya Kiyama wamsute hata Mungu.

Kama kweli tafsiri ni hiyo waisemayo wao Makadiyani kwa nini basi tamko *Rusul* hili lilioko hapa katika Aya hii ambalo ni Jam'u, la kuonyesha wingi (Mitume), ikawa wao wanalifasiri kwa huyo mmoja tu wao

36. Na wale watakaokadhibisha Aya zetu na kuzifanyia kiburi hao watakuwa watu wa Motoni, watakaa humo daima.

وَالَّذِينَ كَذَّبُوا بِآيَاتِنَا وَاسْتَكْبَرُوا عَنْهَا
أُولَٰئِكَ أَصْحَابُ النَّارِ ۖ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿٣٦﴾

37. Basi ni nani dhalimu mkubwa kuliko yule anayemtungia uwongo Mwenyezi Mungu au anayezikadhibisha Aya zake? Hao (hapa duniani) itawafikia sehemu yao aliyowaandikia Mwenyezi Mungu (ya riziki na mengineyo; hawatapokonywa kwa ajili ya ukafiri wao. Watadumu katika hayo) mpaka watakapowafikia wajumbe Wetu kuwafisha. Hapo watawaambia, "Wako wapi mliokuwa mkiwaabudu badala ya Mwenyezi Mungu?" Watasema: "Wametupotea;" na watajishuhudia wenyewe kwamba walikuwa makafiri.

فَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنِ افْتَرَىٰ عَلَى اللَّهِ كَذِبًا أَوْ كَذَّبَ
بِآيَاتِهِ ۚ أُولَٰئِكَ يَنَالُهُمْ نَصِيبُهُمْ مِنَ الْكِتَابِ ۖ
حَتَّىٰ إِذَا جَاءَتْهُمْ رُسُلُنَا يَتَوَفَّوْنَهُمْ قَالُوا أَيْنَ مَا
كُنْتُمْ تَدْعُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ ۖ قَالُوا ضَلُّوا عَنَّا وَ
شَهِدُوا عَلَىٰ أَنْفُسِهِمْ أَنَّهُمْ كَانُوا كَافِرِينَ ﴿٣٧﴾

38. Atasema (Mwenyezi Mungu siku ya Kiyama awaambie): "Ingieni Motoni pamoja na uma zilizopita kabla yenu; za Majini na watu." Kila utakapoingia uma utawalani wenzao. Mpaka watakapokusanyika wote humo, wa nyuma wao (wale waliofuata) watasema kwa ajili ya wa kwanza wao (waliowafuata hata wakapotea) "Mola wetu! Hawa ndio waliotupoteza; basi wape adhabu ya Moto marudufu (yaani zaidi kuliko sisi)" Atasema: "Itakuwa kwenu nyinyi nyote (adhabu) marudufu, lakini nyinyi hamjui tu (bado)."

قَالَ ادْخُلُوا فِي أُمَمٍ قَدْ خَلَتْ مِنْ قَبْلِكُمْ مِنَ
الْجِنِّ وَالْإِنْسِ فِي النَّارِ ۖ كُلَّمَا دَخَلَتْ أُمَّةٌ لَعَنَتْ
أُخْتَهَا ۖ حَتَّىٰ إِذَا ادَّارَكُوا فِيهَا جَمِيعًا قَالَتْ
أُخْرَاهُمْ لِأُولَاهُمْ رَبَّنَا هَٰؤُلَاءِ أَضَلُّونَا فَآتِهِمْ
عَذَابًا ضِعْفًا مِنَ النَّارِ ۖ قَالَ لِكُلٍّ ضِعْفٌ
وَلَٰكِنْ لَا تَعْلَمُونَ ﴿٣٨﴾

39. Na wa kwanza wao watasema kuwaambia wa nyuma wao: "Basi nyinyi pia hamkuwa na fadhila kuliko sisi. (Mmefanya mabaya kama sisi).

وَقَالَتْ أُولَاهُمْ لِأُخْرَاهُمْ فَمَا كَانَ لَكُمْ
عَلَيْنَا مِنْ فَضْلٍ

---

waliompachikia huo utume wa uwongo wauzuwao? Kuna mitume wangapi wa uzushi waliozuka kabla na baada ya huyo wao; basi kwa nini hawawafuati na hao pia na hali ya kuwa Aya hii inasema: Watakapokufikieni Mitume miongoni mwenu (wanaadamu) . . .?"

Basi hicho ni kisingizio chao tu kisichokuwa na nguvu hata chembe — husemi uzi wa buibui. Huvitia mnasoni vijinyama dhaifu tu, tena kwa khadaa; kama wao Makadiyani.

Basi hana ruhusa aliye Mwislamu kuitakidi kuwa baada ya Nabii Muhammad (s.a.w.) atapata Utume mtu mwengine. Akisema hivyo atakuwa Murtadi waachike wake zake, zibatilike zote amali zake.

Ukafiri wao mkubwa wa kumdaia mtu wao Utume wameupachika barabara hapa vile vile, wakajidai kuwa unaweza kufasirika ". . . na haitakuwa kamwe mradi wake kudhania kuwa pengine mwongozo hauwezi kufika . . . mtapata kuaa katika wakati ambao Mjumbe wa Mungu ametokea, msikose kumfuata . . . yanaonyesha kwamba Mitume watakaofika baada ya Mtume Muhammad s.a.w. hawatoleta sharia mpya . . ."

Hapana moja katika haya—na mengine waliyoyadai — lililomo katika Aya hii kama unavyoiona. Lakini basi tu, pupa lao na uchu wao wa kutaka kupoteza Waislamu. Mwenyezi Mungu atatukinga Inshaallah na shari yao. Ukafiri wa kudai Utume baada ya Nabii Muhammad tumekwisha kuutaja katika Maelezo ya Aya ya 7 ya *Suratul Faatihah* na Aya ya 4 ya *Suratul Baqarah*.

37. Kama hao Makadiyani wanaomsingizia uwongo Mwenyezi Mungu kuwa amempa Utume Ghulam Ahmad Mirza. Hasha lillah.

38. Kila mmoja atapata adhabu kwa mengi. Atapata adhabu marudufu.

Wale waliopotezwa watapata adhabu ya (a) kukubali kupotezwa, na hali ya kuwa wamepewa akili ya kutambua mema na mabaya. Na watapata adhabu ya (b) Kufanya hayo mabaya. Na watapata adhabu ya (c) Kuwarithisha watu wao mabaya. Na . . .

Na wale waliopoteza watapata adhabu ya (a) Kufanya wao mabaya na ya (b) Kupoteza hao waliowapoteza na ya

فَذُوقُوا الْعَذَابَ بِمَا كُنْتُمْ تَكْسِبُونَ ﴿٣٩﴾

Kwa hivyo onjeni adhabu kwa sababu ya yale (maasi) mliyokuwa mkiyachuma (kama sisi)."

إِنَّ الَّذِينَ كَذَّبُوا بِآيَاتِنَا وَاسْتَكْبَرُوا عَنْهَا لَا
تُفَتَّحُ لَهُمْ أَبْوَابُ السَّمَاءِ وَلَا يَدْخُلُونَ
الْجَنَّةَ حَتَّىٰ يَلِجَ الْجَمَلُ فِي سَمِّ الْخِيَاطِ ۚ
وَكَذَٰلِكَ نَجْزِي الْمُجْرِمِينَ ﴿٤٠﴾

40. Hakika wale wanaozikadhibisha Aya zetu na kuzifanyia kiburi (hawataki kuzifuata), hawatafunguliwa milango ya mbingu, wala hawataingia Peponi mpaka aingie ngamia katika tundu ya sindano; (na haya ni muhali). Na hivi ndivyo tunavyowalipa waovu.

لَهُمْ مِنْ جَهَنَّمَ مِهَادٌ وَمِنْ فَوْقِهِمْ غَوَاشٍ ۚ
وَكَذَٰلِكَ نَجْزِي الظَّالِمِينَ ﴿٤١﴾

41. Watakuwa na magodoro ya moto wa Jahanamu; na juu yao nguo za kujifunika (za moto wa Jahanamu). Na hivi ndivyo tunavyowalipa madhalimu.

وَالَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَا نُكَلِّفُ نَفْسًا
إِلَّا وُسْعَهَا أُولَٰئِكَ أَصْحَابُ الْجَنَّةِ ۖ هُمْ فِيهَا
خَالِدُونَ ﴿٤٢﴾

42. Na wale wanaoamini na kufanya vitendo vizuri — hatumkalifishi mtu yo yote ila kwa kiasi cha uweza wake — hao ndio watu wa Peponi. Wao watakaa humo daima.

وَنَزَعْنَا مَا فِي صُدُورِهِمْ مِنْ غِلٍّ تَجْرِي
مِنْ تَحْتِهِمُ الْأَنْهَارُ ۖ وَقَالُوا الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي
هَدَانَا لِهَٰذَا وَمَا كُنَّا لِنَهْتَدِيَ لَوْلَا أَنْ هَدَانَا
اللَّهُ ۖ لَقَدْ جَاءَتْ رُسُلُ رَبِّنَا بِالْحَقِّ ۖ وَنُودُوا
أَنْ تِلْكُمُ الْجَنَّةُ أُورِثْتُمُوهَا بِمَا كُنْتُمْ
تَعْمَلُونَ ﴿٤٣﴾

43. Na tutaiondoa bughudha vifuani mwao (Wawe wanapendana wote kweli kweli); mbele yao iwe inapita mito. Na watasema (katika kushukuru kwao); "Sifa zote njema zinamstahikia Mwenyezi Mungu ambaye ametuongoza katika (neema) hizi. Na hatukuwa wenye kuongoka wenyewe kama asingetuongoza Mwenyezi Mungu. Mitume wa Mola wetu wameleta haki." Na watanadiwa (wataambiwa) ya kwamba: "Hii ndiyo Pepo mliyorithishwa kwa sababu ya yale mliyokuwa mkiyafanya."

وَنَادَىٰ أَصْحَابُ الْجَنَّةِ أَصْحَابَ النَّارِ أَنْ قَدْ
وَجَدْنَا مَا وَعَدَنَا رَبُّنَا حَقًّا فَهَلْ وَجَدْتُمْ مَا
وَعَدَ رَبُّكُمْ حَقًّا ۖ قَالُوا نَعَمْ ۚ فَأَذَّنَ مُؤَذِّنٌ
بَيْنَهُمْ أَنْ لَعْنَةُ اللَّهِ عَلَى الظَّالِمِينَ ﴿٤٤﴾

44. Na watu wa Peponi wataweta watu wa Motoni (waseme): "Sisi tumekuta aliyotuahidi Mola wetu kuwa ni kweli. Je, na nyinyi (pia) mumekuta aliyokuahidini Mola wenu kuwa ni kweli?" Watasema (watu wa Motoni). "Ndiyo," Basi mtangazaji atatangaza baina yao (aseme): "Laana ya Mwenyezi Mungu iko juu ya madhalimu (waliodhulumu nafsi zao)

---

(c) Kuendeleza mabaya mpaka yatakapofika; na . . .

44. Masafa ya baina ya mahala uiapokuwa Moto na itapokuwako Pepo ni ya umbali usiohisika wala kukadirika. Hauingii akilini. Na juu ya hivi watu wa Peponi wataweza kuwasemesha watu wa Motoni na wawasikie; na wa Motoni kuwasemesha watu wa Peponi na wawasikie.

Kabla ya kuvumbuliwa Maredio haya *(Broadcasting)* wasiokuwa Waislamu wakiona upuzi maneno hayo na ni uwongo pia. Vipi baina ya masafa hayo viumbe watasikilizana!

Lakini waliokuwa Waislamu waliamini, kwa kuwa Mwenyezi Mungu amesema hivyo na kuwa Mwenyezi Mungu amesema vile vile kuwa haya yanayosemwa na Uislamu yakaonekana uwongo, yatadhihiri ukweli wake hapa hapa duniani katika pande zote za ulimwengu. Alisema habari hii katika Aya ya 53 ya *Sura Haa Mym Sajdah.*

Basi sasa tunaona ukweli wake huu. Mtu anasema London anasikilizana hapa Afrika; kiasi cha meli tisaa alfu! Bali anasema America na Rusi na China na . . . na akasikilizana.

Basi si hii shahada moja katika shahada za kuonyesha kuwa kweli Qurani amesema Mwenyezi Mungu ambaye

الَّذِينَ يَصُدُّونَ عَن سَبِيلِ اللَّهِ وَيَبْغُونَهَا عِوَجًا ۚ وَهُم بِالْآخِرَةِ كَافِرُونَ ﴿٤٥﴾

45. Ambao walikuwa wakizuilia (watu) na njia ya Mwenyezi Mungu na wakataka kuipotosha, (watu waione potofu), na wakawa hawaamini Akhera.

وَبَيْنَهُمَا حِجَابٌ ۚ وَعَلَى الْأَعْرَافِ رِجَالٌ يَعْرِفُونَ كُلًّا بِسِيمَاهُمْ ۚ وَنَادَوْا أَصْحَابَ الْجَنَّةِ أَن سَلَامٌ عَلَيْكُمْ ۚ لَمْ يَدْخُلُوهَا وَهُمْ يَطْمَعُونَ ﴿٤٦﴾

46. Na baina yao (hao watu wa Peponi na Motoni) kutakuwa na mahali pa watu wengine (watu ambao bado hawajasamehewa vijidhambi vyao vidogo ili wende Peponi). Na juu ya mahala hapo palipoinuka watakuwako watu hao watakaowafahamu wote (wa Peponi na Motoni) kwa alama zao; na watawaita watu wa Peponi (kuwaambia): "Assalamu Alaykum" (amani iwe juu yenu)." . Wao (wenye vijidhambi hivyo) bado hawajaingia humo (Peponi) lakini wanatumai.

وَإِذَا صُرِفَتْ أَبْصَارُهُمْ تِلْقَاءَ أَصْحَابِ النَّارِ قَالُوا رَبَّنَا لَا تَجْعَلْنَا مَعَ الْقَوْمِ الظَّالِمِينَ ﴿٤٧﴾

47. Na macho yao yanapogeuzwa kwenye watu wa Motoni, husema: "Mola wetu! Usituweke pamoja na watu madhalimu (hawa; tusamehe makosa yetu tuingie Peponi)."

وَنَادَىٰ أَصْحَابُ الْأَعْرَافِ رِجَالًا يَعْرِفُونَهُم بِسِيمَاهُمْ قَالُوا مَا أَغْنَىٰ عَنكُمْ جَمْعُكُمْ وَمَا كُنتُمْ تَسْتَكْبِرُونَ ﴿٤٨﴾

48. Na hao wa mahali paliponyanyuka watawaita watu (wa Motoni) wanaowafahamu kwa alama zao, waseme: "Haukukusaidieni wingi wenu (huko) wala (vile) mlivyokuwa mkijivunia."

أَهَٰؤُلَاءِ الَّذِينَ أَقْسَمْتُمْ لَا يَنَالُهُمُ اللَّهُ بِرَحْمَةٍ ۚ ادْخُلُوا الْجَنَّةَ لَا خَوْفٌ عَلَيْكُمْ وَلَا أَنتُمْ تَحْزَنُونَ ﴿٤٩﴾

49. (Wazidi kuwasimanga kwa kuwaambia). "Je, hawa (waliotiwa Peponi) sio wale mliokuwa mkiwaapia kwamba Mwenyezi Mungu hatawafikishia rehema? (Mnaona sasa; wameambiwa) "Ingieni Peponi, hakuna khofu juu yenu, wala hamtahuzunika."

وَنَادَىٰ أَصْحَابُ النَّارِ أَصْحَابَ الْجَنَّةِ أَنْ أَفِيضُوا عَلَيْنَا مِنَ الْمَاءِ أَوْ مِمَّا رَزَقَكُمُ اللَّهُ ۚ قَالُوا إِنَّ اللَّهَ حَرَّمَهُمَا عَلَى الْكَافِرِينَ ﴿٥٠﴾

50. Na watu wa Motoni watawaita watu wa Peponi, (kuwaambia): "Tumiminieni (Tumwagieni) maji au (kitu) katika vile alivyokupeni Mwenyezi Mungu." Waseme (watu wa Peponi): "Hakika Mwenyezi Mungu ameviharimisha vyote viwili hivyo kwa makafiri."

الَّذِينَ اتَّخَذُوا دِينَهُمْ لَهْوًا وَلَعِبًا وَغَرَّتْهُمُ الْحَيَاةُ الدُّنْيَا ۚ فَالْيَوْمَ نَنسَاهُمْ كَمَا نَسُوا لِقَاءَ يَوْمِهِمْ هَٰذَا وَمَا كَانُوا بِآيَاتِنَا يَجْحَدُونَ ﴿٥١﴾

51. "Ambao waliifanya dini yao kuwa upuzi na mchezo, na maisha ya dunia yakawadanganyia." Basi leo Sisi tunawasahau (tutawaacha Motoni) kama walivyosahau mkutano wa siku yao hii, na kwa sababu ya kule kuzikataa Aya zetu.

وَلَقَدْ جِئْنَاهُم بِكِتَابٍ فَصَّلْنَاهُ عَلَىٰ عِلْمٍ هُدًى وَرَحْمَةً لِّقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ ﴿٥٢﴾

52. Na tumewaletea Kitabu tulichokipambanua vizuri kwa ujuzi (wetu), ambacho ni uwongofu na rehema kwa watu wanaoamini.

---

halimfichikii jambo katika yaliyopita na yanayokuja?

Na sisi hapa petu Africa baada ya muda kidogo tutawasikilizisha vizuri sauti zetu kama wanavyotusikilizisha zao. Na tumekwisha kuanza kuwasikilizisha baadhi yao.

Bali Qurani ilibashiri tangu miaka hiyo zaidi ya miaka 1390 leo kuwa "Si wataweza kusemezana tu bali wataweza kuonana na kupeana khasa" kama Aya hii ya 46 na ya 48 na ya 50 zinavyosema.

Na sasa zimekwishakuja *Television* za kuthibitisha haya.

51. Zinatajwa baadhi ya sifa za hao wabaya.

53. Hawatazamii ila matokeo yake. (Nayo yatatokea). Siku yatakapotokea matokeo yake hayo watasema wale waliopuza hapo zamani: "Kweli Mitume wa Mola wetu walileta haki; (tunakubali sasa). Je, tunao waombezi ili watuombee? Au tutarudishwa ili tufanye yasiyokuwa yale tuliyokuwa tukiyafanya?" Bila shaka wamezitia nafsi zao khasarani, na umewapotea ule uwongo waliokuwa wakiutunga.

هَلْ يَنظُرُونَ إِلَّا تَأْوِيلَهُ ۚ يَوْمَ يَأْتِي تَأْوِيلُهُ
يَقُولُ الَّذِينَ نَسُوهُ مِن قَبْلُ قَدْ جَاءَتْ رُسُلُ
رَبِّنَا بِالْحَقِّ ۚ فَهَل لَّنَا مِن شُفَعَاءَ فَيَشْفَعُوا
لَنَا أَوْ نُرَدُّ فَنَعْمَلَ غَيْرَ الَّذِي كُنَّا نَعْمَلُ ۚ قَدْ
خَسِرُوا أَنفُسَهُمْ وَضَلَّ عَنْهُم مَّا كَانُوا يَفْتَرُونَ ﴿٥٣﴾

54. Hakika Mola wenu ni Mwenyezi Mungu aliyeziumba mbingu na ardhi kwa siku sita. Kisha akatawala juu ya Arshi yake. Huufunika usiku kwa mchana, uufuatiao upesi upesi, (na huufunika mchana kwa usiku uufuatiao upesi upesi). Na (ameliumba) jua na mwezi na nyota. (Na vyote) vimetiishwa kwa amri Yake (Mwenyezi Mungu viwe vya manufaa makubwa nanyi). Fahamuni. Kuumba (ni Kwake tu Mwenyewe Mwenyezi Mungu) na amri zote ni zake (Mwenyezi Mungu). Ametukuka kabisa Mwenyezi Mungu, Mola wa walimwengu wote.

إِنَّ رَبَّكُمُ اللَّهُ الَّذِي خَلَقَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ
فِي سِتَّةِ أَيَّامٍ ثُمَّ اسْتَوَىٰ عَلَى الْعَرْشِ يُغْشِي
اللَّيْلَ النَّهَارَ يَطْلُبُهُ حَثِيثًا وَالشَّمْسَ وَالْقَمَرَ
وَالنُّجُومَ مُسَخَّرَاتٍ بِأَمْرِهِ ۗ أَلَا لَهُ الْخَلْقُ وَالْأَمْرُ ۗ
تَبَارَكَ اللَّهُ رَبُّ الْعَالَمِينَ ﴿٥٤﴾

55. Mwombeni Mola wenu kwa unyenyekevu na kwa siri kwa sauti ndogo bila ya kufanya kelele). Yeye (Mwenyezi Mungu) hawapendi wapitao mipaka.

ادْعُوا رَبَّكُمْ تَضَرُّعًا وَخُفْيَةً ۚ إِنَّهُ لَا يُحِبُّ
الْمُعْتَدِينَ ﴿٥٥﴾

56. Wala msifanye uharibifu katika nchi baada ya kuwa imekwisha kutengenezwa. Na mwombeni kwa kuogopa na kwa kutumai. Bila shaka rehema ya Mwenyezi Mungu iko karibu sana na (wale waja wake) wanaofanya mema.

وَلَا تُفْسِدُوا فِي الْأَرْضِ بَعْدَ إِصْلَاحِهَا وَادْعُوهُ خَوْفًا
وَطَمَعًا ۚ إِنَّ رَحْمَتَ اللَّهِ قَرِيبٌ مِّنَ الْمُحْسِنِينَ ﴿٥٦﴾

57. Na yeye ndiye apelekaye pepo kuwa bishara (habari njema) kabla ya kufika rehema yake (mvua). Hata hizo pepo zinapobeba mawingu mazito tunayapeleka katika mji uliokufa. Kisha tunateremsha hapo maji kwa (mawingu) hayo. Kwa hayo tukaotesha kila (aina ya) matunda. Basi namna hivi tutawafufua wafu, ili mpate kukumbuka.

وَهُوَ الَّذِي يُرْسِلُ الرِّيَاحَ بُشْرًا بَيْنَ يَدَيْ
رَحْمَتِهِ ۖ حَتَّىٰ إِذَا أَقَلَّتْ سَحَابًا ثِقَالًا سُقْنَاهُ
لِبَلَدٍ مَّيِّتٍ فَأَنزَلْنَا بِهِ الْمَاءَ فَأَخْرَجْنَا بِهِ
مِن كُلِّ الثَّمَرَاتِ ۚ كَذَٰلِكَ نُخْرِجُ الْمَوْتَىٰ لَعَلَّكُمْ
تَذَكَّرُونَ ﴿٥٧﴾

---

53. Yanatajwa mahangaiko yatakaowafika waovu.

55. Dua zetu za kumwomba Mwenyezi Mungu tunaambiwa tumwombe kwa unyenyekevu bila ya makelele, na sisi hatusikii—makelele tu moto mmoja. Si kelele zinazosikilizana msikiti wa Ijumaa siku ya Ijumaa za wasomaji, hali ya kuwa wanapata dhambi kwa ajili ya kuwababaisha wanaosali. Si kelele zinazofanywa misikitini kila siku, za nyuradi za Sala na nyenginezo. Si kelele za Amina hiyo ya *Alhamdu* na *Amina* ya *Qunut* na nyinginezo. Si kelele za . . . Almuradi mashindano ya kelele. Kila mmoja anajitahidi ili kelele zake ziwe kubwa kuliko za mwenziwe na kuhimizwa kuwa "Pasukeni vifua vyenu," na hali ya kuwa Mtume amesema: "Zioneeni huruma nafsi zenu. Nyinyi hamumsemezi kiziwi!" Yamebadilishwa mambo: Siyo imekuwa ndiyo.

56. Rehema za Mwenyezi Mungu huwafika wale wenye rehema na huruma juu ya viumbe wenziwe. Asiyewafanyia wenziwe huruma naye hatafanyiwa na Mwenyezi Mungu. Basi natujitahidi kuwasaidia wanyonge na wahitaji mwisho wa jitihada yetu. Ikiwa si hivyo rehema ya Mwenyezi Mungu itakuwa mbali na sisi hiyo Siku ya Siku. Amesema Mtume: "Warehemuni hawa walioko hapa katika ardhi mpate kurehemewa huko Mbinguni." "Mwenyezi Mungu huwarehemu wale wanaorehemu wenzao."

58. Na nchi nzuri hutoa mimea yake (upesi) kwa idhini ya Mola wake. Na nchi iliyo mbaya haitoi (mimea yake) ila kwa taabu tu. Namna hivi tunazipambanua Aya kwa watu wanaoshukuru.

وَالْبَلَدُ الطَّيِّبُ يَخْرُجُ نَبَاتُهُ بِإِذْنِ رَبِّهِ ۚ وَالَّذِي خَبُثَ لَا يَخْرُجُ إِلَّا نَكِدًا ۚ كَذَٰلِكَ نُصَرِّفُ الْآيَاتِ لِقَوْمٍ يَشْكُرُونَ ﴿٥٨﴾ ع

59. Tulimpeleka Nuhu kwa watu wake, naye akasema: "Enyi watu wangu! Muabuduni Mwenyezi Mungu. Nyinyi hamna Mungu ila Yeye. Hakika mimi ninakukhofieni adhabu ya siku (hiyo) iliyo kuu."

لَقَدْ أَرْسَلْنَا نُوحًا إِلَىٰ قَوْمِهِ فَقَالَ يَا قَوْمِ اعْبُدُوا اللَّهَ مَا لَكُم مِّنْ إِلَٰهٍ غَيْرُهُ إِنِّي أَخَافُ عَلَيْكُمْ عَذَابَ يَوْمٍ عَظِيمٍ ﴿٥٩﴾

60. Wakuu wa watu wake wakasema: "Sisi tunakuona umo katika upotofu (upotevu) ulio dhahiri (kwa kutukataza haya tuliyowakuta nayo wazee wetu)."

قَالَ الْمَلَأُ مِن قَوْمِهِ إِنَّا لَنَرَاكَ فِي ضَلَالٍ مُّبِينٍ ﴿٦٠﴾

61. Akasema: "Enyi kaumu yangu! Mimi simo katika upotofu (upotevu) lakini mimi ni Mtume nitokaye kwa Mola wa walimwengu wote."

قَالَ يَا قَوْمِ لَيْسَ بِي ضَلَالَةٌ وَلَٰكِنِّي رَسُولٌ مِّن رَّبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٦١﴾

62. "Nakufikishieni ujumbe wa Mola wangu na ninakunasihini; na ninayajua kwa Mwenyezi Mungu msiyoyajua."

أُبَلِّغُكُمْ رِسَالَاتِ رَبِّي وَأَنصَحُ لَكُمْ وَأَعْلَمُ مِنَ اللَّهِ مَا لَا تَعْلَمُونَ ﴿٦٢﴾

63. "Je, mnastaajabu kukufikieni mauidha yanayotoka kwa Mola wenu kwa njia ya mtu aliye ni mmoja katika nyinyi, (aliyekuja) ili akuonyeni na ili mwogope na ili mpate kurehemewa?"

أَوَعَجِبْتُمْ أَن جَاءَكُمْ ذِكْرٌ مِّن رَّبِّكُمْ عَلَىٰ رَجُلٍ مِّنكُمْ لِيُنذِرَكُمْ وَلِتَتَّقُوا وَلَعَلَّكُمْ تُرْحَمُونَ ﴿٦٣﴾

64. Walimkadhibisha (tu). Basi tukamokoa yeye na waliokuwa pamoja naye katika jahazi. Na tukawazamisha wale waliozikadhibisha Aya zetu. Bila shaka hao walikuwa watu vipofu.

فَكَذَّبُوهُ فَأَنجَيْنَاهُ وَالَّذِينَ مَعَهُ فِي الْفُلْكِ وَأَغْرَقْنَا الَّذِينَ كَذَّبُوا بِآيَاتِنَا ۚ إِنَّهُمْ كَانُوا قَوْمًا عَمِينَ ﴿٦٤﴾ ع

65. Na kwa Adi (tulimpeleka) ndugu yao, Hudi Akasema: "Enyi kaumu yangu! Muabuduni Mwenyezi Mungu; nyinyi hamna mungu ila yeye. Basi hamuogopi?"

وَإِلَىٰ عَادٍ أَخَاهُمْ هُودًا ۚ قَالَ يَا قَوْمِ اعْبُدُوا اللَّهَ مَا لَكُم مِّنْ إِلَٰهٍ غَيْرُهُ ۚ أَفَلَا تَتَّقُونَ ﴿٦٥﴾

66. Wakasema wakuu waliokufuru katika kaumu yake; "Sisi tunakuona umo katika upumbavu na tunakuona u miongoni mwa waongo."

قَالَ الْمَلَأُ الَّذِينَ كَفَرُوا مِن قَوْمِهِ إِنَّا لَنَرَاكَ فِي سَفَاهَةٍ وَإِنَّا لَنَظُنُّكَ مِنَ الْكَاذِبِينَ ﴿٦٦﴾

---

57. Kama Mwenyezi Mungu anavyofufua kwa mvua ardhi iliyokufa ndivyo atakavyowafufua wafu kwa hicho atakachowafufulia.

58. Basi na watu wabaya ndivyo vivyo hivyo; ni taabu kuwaleta katika kheri. Lakini tusichoke wala tusikate tamaa. Watapatikana watakaotengenea.

59. Tangu hapa mpaka karibu na mwisho wa sura vinatajwa visa vya baadhi ya Mitume na kaumu zao.

64. Kisa cha Nabii Nuhu kinaelezwa kila mara. Na kitatajwa mara nyingi kwa urefu kuliko hivi. Na huyo Nabii Nuhu ni Mtume wa zamani kabisa. Yeye aliwalingania watu waliokuwa Iraqi. Na takriba Ulimwengu wote wa zama hizo na ustarabu wake ulikuwa huko Iraqi, kama tunavyosoma katika vitabu vya Tarekhe. Na Mtume mkubwa aliyemtangulia ni Nabii Idrisi tu. Na yeye alikuwa Misri. Na Misri na Iraqi ndizo nchi za mwanzo kuwa ni miji kisha zikawa na ustaarabu. Ilitangulia Misri ikafuatiwa na Iraqi.

65. Hawa Kina Adi walikuwa wakikaa kusini ya Bara Arabu huko Hadhramout na Yamen, sehemu ambayo hapo zamani sana ilikuwa na miji mikubwa na ustaarabu mkubwa sana unaokaribia huo wa Iraqi na Misri. Basi

قَالَ يٰقَوْمِ لَيْسَ بِيْ سَفَاهَةٌ وَّلٰكِنِّيْ رَسُوْلٌ مِّنْ رَّبِّ الْعٰلَمِيْنَ ﴿٦٧﴾

67. Akasema: "Enyi kaumu yangu! Mimi sina upumbavu. Lakini mimi ni Mtume niliyetoka kwa Mola wa walimwengu."

اُبَلِّغُكُمْ رِسٰلٰتِ رَبِّيْ وَاَنَا لَكُمْ نَاصِحٌ اَمِيْنٌ ﴿٦٨﴾

68. "Nakufikishieni ujumbe wa Mola wangu. Na mimi kwenu ni (mtu) nasihi muaminifu."

اَوَعَجِبْتُمْ اَنْ جَآءَكُمْ ذِكْرٌ مِّنْ رَّبِّكُمْ عَلٰى رَجُلٍ مِّنْكُمْ لِيُنْذِرَكُمْ ؕ وَاذْكُرُوْٓا اِذْ جَعَلَكُمْ خُلَفَآءَ مِنْۢ بَعْدِ قَوْمِ نُوْحٍ وَّزَادَكُمْ فِى الْخَلْقِ بَصْطَةً ۚ فَاذْكُرُوْٓا اٰلَآءَ اللّٰهِ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُوْنَ ﴿٦٩﴾

69. "Mnaona ajabu kukufikieni mauidha yanayotoka kwa Mola wenu kwa (ulimi wa) mtu aliye mmoja katika nyinyi ili akuonyeni? (Mwabuduni Mwenyezi Mungu) na mkumbuke alivyokufanyeni makhalifa baada ya watu wa Nuh. (Mkawa nyinyi washikaji mahala pao). Na akakuzidisheni sana katika umbo. Basi zikumbukeni neema za Mwenyezi Mungu ili mpate kufaulu."

قَالُوْٓا اَجِئْتَنَا لِنَعْبُدَ اللّٰهَ وَحْدَهٗ وَنَذَرَ مَا كَانَ يَعْبُدُ اٰبَآؤُنَا ۚ فَاْتِنَا بِمَا تَعِدُنَآ اِنْ كُنْتَ مِنَ الصّٰدِقِيْنَ ﴿٧٠﴾

70. Wakasema: "Je! Umetujia ili tumuabudu Mwenyezi Mungu peke yake na tuyaache waliyokuwa wakiyaabudu baba zetu? Basi tuletee unayotuahidi ukiwa ni miongoni mwa wasemao kweli. (Lakini hayo hatuyafuati)."

قَالَ قَدْ وَقَعَ عَلَيْكُمْ مِّنْ رَّبِّكُمْ رِجْسٌ وَّغَضَبٌ ؕ اَتُجَادِلُوْنَنِيْ فِيْٓ اَسْمَآءٍ سَمَّيْتُمُوْهَآ اَنْتُمْ وَاٰبَآؤُكُمْ مَّا نَزَّلَ اللّٰهُ بِهَا مِنْ سُلْطٰنٍ ؕ فَانْتَظِرُوْٓا اِنِّيْ مَعَكُمْ مِّنَ الْمُنْتَظِرِيْنَ ﴿٧١﴾

71. Akasema: "Bila shaka adhabu na ghadhabu zimekwisha kukuangukieni kutoka kwa Mola wenu. Mnanijadili kwa ajili ya majina (tu) mliyoyaita (masanamu hayo) nyinyi na baba zenu (kuwa ni waungu) ambayo Mwenyezi Mungu hakuyateremshia dalili? Basi ngojeni; mimi pia ni pamoja nanyi katika wangojao."

فَاَنْجَيْنٰهُ وَالَّذِيْنَ مَعَهٗ بِرَحْمَةٍ مِّنَّا وَقَطَعْنَا دَابِرَ الَّذِيْنَ كَذَّبُوْا بِاٰيٰتِنَا وَمَا كَانُوْا مُؤْمِنِيْنَ ﴿٧٢﴾

72. Basi tukamuokoa yeye na waliokuwa pamoja naye kwa rehema zetu, na tukakata mizizi ya wale waliozikadhibisha Aya zetu, na (ambao) hawakuwa wenye kuamini."

وَاِلٰى ثَمُوْدَ اَخَاهُمْ صٰلِحًا ۘ قَالَ يٰقَوْمِ اعْبُدُوا اللّٰهَ مَا لَكُمْ مِّنْ اِلٰهٍ غَيْرُهٗ ؕ قَدْ جَآءَتْكُمْ بَيِّنَةٌ مِّنْ رَّبِّكُمْ ؕ هٰذِهٖ نَاقَةُ اللّٰهِ لَكُمْ اٰيَةً فَذَرُوْهَا تَاْكُلْ فِيْٓ اَرْضِ اللّٰهِ وَلَا تَمَسُّوْهَا بِسُوْٓءٍ فَيَاْخُذَكُمْ عَذَابٌ اَلِيْمٌ ﴿٧٣﴾

73. Na kwa Thamud (tulimpeleka) ndugu yao, Saleh. Akasema: "Enyi watu wangu! Muabuduni Mwenyezi Mungu, Nyinyi hamna Mola ila Yeye. Hakika umekwisha kukufikieni muujiza ulio dhahiri kutoka kwa Mola wenu. Huyu ni ngamia jike wa Mwenyezi Mungu aliye ni Ishara kwenu (ya Utume wangu). Basi muacheni ale katika ardhi ya Mungu, wala msimtie katika dhara yo yote, isije ikakushikeni adhabu iumizayo."

---

walipelekewa huyo Mtume aliyekuwa akiitwa Nabii Hudi. Naye alikuwa wa kabila moja na wao. Na huyo Nabii Hudi ndiye Mtume mkubwa aliyemfuatia Nabii Nuhu.

73-Hawa Kina Thamud walikuwa wakikaa kaskazini ya Bara Arabu. Waliurithi ustaarabu wa wenzao—Kina Adi—waliokuwa kusini ya Bara Arabu. Wakapelekewa Mtume wa kabila moja na wao, aliyekuwa akitwa Saleh.

Katika mazonge yao waliomtilia Mtume wao huyu ni kumwambia 'Kama wewe ni Mtume basi liamrishe jabali hili lipasuke. Na likipasuka atoke ngamia mwenye mimba pevu; na papo hapo azae. Ukifanya hivi tutasadiki kuwa kweli wewe ni Mtume. Ama ikiwa si hivi basi hatukuamini.'

Nabii Saleh akaomba Mwenyezi Mungu; ukatokea muujiza huu waliutaka. Lakini wapi! Hawakuamini; ila walimtafutia fursa wakamuua.

74. "Na kumbukeni (Mwenyezi Mungu) alivyokufanyeni makhalifa baada ya Adi na kukuwekeni vizuri katika ardhi; mnajenga majumba makubwa ya kifalme katika nyanda zake, na mnachonga majumba katika majabali (yake). Basi zikumbukeni neema za Mwenyezi Mungu, wala msifisidi katika ardhi kwa kufanya uharibifu."

وَاذْكُرُوٓا إِذْ جَعَلَكُمْ خُلَفَآءَ مِنۢ بَعْدِ عَادٍ وَبَوَّأَكُمْ فِى الْأَرْضِ تَتَّخِذُونَ مِن سُهُولِهَا قُصُورًا وَتَنْحِتُونَ الْجِبَالَ بُيُوتًا ۖ فَاذْكُرُوٓا ءَالَآءَ اللَّهِ وَلَا تَعْثَوْا فِى الْأَرْضِ مُفْسِدِينَ ﴿٧٤﴾

75. Wakasema wakuu wa kaumu yake waliotakabari, kuwaambia wale walio dhaifu wenye kuamini miongoni mwao: "Je,! Mnaitakidi ya kwamba Saleh ametumwa (amepewa Utume) na Mola wake?" Wakasema: "Hakika tunayaamini yale aliyotumwa (kuyafikisha)."

قَالَ الْمَلَأُ الَّذِينَ اسْتَكْبَرُوا مِن قَوْمِهِۦ لِلَّذِينَ اسْتُضْعِفُوا لِمَنْ ءَامَنَ مِنْهُمْ أَتَعْلَمُونَ أَنَّ صَٰلِحًا مُّرْسَلٌ مِّن رَّبِّهِۦ ۚ قَالُوٓا إِنَّا بِمَآ أُرْسِلَ بِهِۦ مُؤْمِنُونَ ﴿٧٥﴾

76. Wakasema wale waliotakabari: "Sisi tunayakataa yale mnayoyaamini."

قَالَ الَّذِينَ اسْتَكْبَرُوٓا إِنَّا بِالَّذِىٓ ءَامَنتُم بِهِۦ كَٰفِرُونَ ﴿٧٦﴾

77. Na wakamtumbua (wakamwua) yule ngamia na wakaasi amri ya Mola wao na wakasema: "Ee Saleh! Tuletee unayotuahidi ikiwa wewe ni miongoni mwa Mitume."

فَعَقَرُوا النَّاقَةَ وَعَتَوْا عَنْ أَمْرِ رَبِّهِمْ وَقَالُوا يَٰصَٰلِحُ ائْتِنَا بِمَا تَعِدُنَآ إِن كُنتَ مِنَ الْمُرْسَلِينَ ﴿٧٧﴾

78. Mtetemeko wa ardhi ukawanyakuwa (roho zao) na wakawa wamekufa humo katika miji yao.

فَأَخَذَتْهُمُ الرَّجْفَةُ فَأَصْبَحُوا فِى دَارِهِمْ جَٰثِمِينَ ﴿٧٨﴾

79. Basi (Saleh) akawaacha (akenda zake), na huku anasema: "Enyi kaumu yangu! Nilikufikishieni ujumbe wa Mola wangu na nikakunasihini, lakini nyinyi hamwapendi wenye nasaha."

فَتَوَلَّىٰ عَنْهُمْ وَقَالَ يَٰقَوْمِ لَقَدْ أَبْلَغْتُكُمْ رِسَالَةَ رَبِّى وَنَصَحْتُ لَكُمْ وَلَٰكِن لَّا تُحِبُّونَ النَّٰصِحِينَ ﴿٧٩﴾

80. Na (tulimpeleka) Luti. Basi (wakumbushe watu wako) alipowaambia kaumu yake: "Je! Mnafanya jambo chafu ambalo hajakutangulieni yoyote kwa (jambo chafu) hilo katika walimwengu!"

وَلُوطًا إِذْ قَالَ لِقَوْمِهِۦٓ أَتَأْتُونَ الْفَٰحِشَةَ مَا سَبَقَكُم بِهَا مِنْ أَحَدٍ مِّنَ الْعَٰلَمِينَ ﴿٨٠﴾

---

Katika hii Aya waliyoifanya ya 74 wametia ukafiri wao wa kukataa muujiza uliokuwa na uliopatikana kwa yule ngamia walioletewa watu wa Nabii Saleh. Wakasema:– "Naye alikuwa ni mnyama tu kama ngamia wengine." Na kuwa "Nabii Saleh alikuwa akisafiri kwenda huko na huko kukhubiri juu ya huyo ngamia wake. Basi aliwaambia watu wake ya kuwa kumzuwia ngamia wake ni kuzuia kazi ya Mwenyezi Mungu anayoifanya." Na hali ya kuwa Mwenyezi Mungu anaonyesha katika chungu ya Aya za Qurani kuwa aliletwa kwa muujiza na akaonyesha miujiza; wao wanamkaidi Mwenyezi Mungu na kumsuta na kumsusuwika na kumwambia kuwa alikuwa ngamia tu akimpanda Nabii Saleh. Mwenyezi Mungu anasema katika Aya hii ya 73 ya *Suratul Aaraf* na Aya ya 64 ya *Surat Hud* kuwa: "Umekwisha kukufikieni muujiza ulio dhahiri kutoka kwa Mola wenu. Huyu ni ngamia jike wa Mwenyezi Mungu aliye ni ishara kwenu (ya Utume wangu)" Wao wanasema ni ngamia tu wa kupanda. Na anasema tena Mwenyezi Mungu katika Aya ya 59 ya *Bani Israili* "Na tuliwapa Wathamudi ngamia jike kuwa ishara iliyo dhahiri (muujiza)" Na anasema katika Aya ya 27 ya *Suratul Qamar:* "Tutawaletea ngamia jike ili kuwajaribu." (muujiza). Na akasema katika Aya ya 155 ya *Suratush Shuaraa:* "Huyu ngamia jike; awe na zamu yake ya kunywa, na nyinyi muwe na zamu yenu ya kuteka katika siku maalumu" ya-ani yeye ana kinywea chake (siku yake nzima makhsusi) na nyinyi mna kinywea chenu cha siku yenu nzima maalumu. Siku yake atamaliza maji ya visima vyote. Si muujiza huu? Ni ngamia wa dasturi tu huyu wa kupanda? Enyi watu nyi!

80. Hawa watu waliopelekewa Nabii Luti akawaonye kwa mabaya yao na awafundishe mema, walikuwa

81. "Nyinyi mnawaendea wanaume kwa kuwa ndio mnaowatamani badala ya wanawake! Ama nyinyi ni watu wafujaji."

إِنَّكُمْ لَتَأْتُونَ الرِّجَالَ شَهْوَةً مِّن دُونِ النِّسَاءِ ۚ
بَلْ أَنتُمْ قَوْمٌ مُّسْرِفُونَ ﴿٨١﴾

82. Na hayakuwa majibu ya kaumu yake isipokuwa kuambizana: "Wafukuzeni katika mji wenu, maana hao ni watu wanaojitakasa (hawataki haya machafu tunayoyafanya. Basi nawatoke. Wanakalia nini?"

وَمَا كَانَ جَوَابَ قَوْمِهِ إِلَّا أَن قَالُوا أَخْرِجُوهُم
مِّن قَرْيَتِكُمْ ۖ إِنَّهُمْ أُنَاسٌ يَتَطَهَّرُونَ ﴿٨٢﴾

83. Basi tukamuokoa yeye (Luti) na watu wake isipokuwa mke wake, alikuwa miongoni mwa waliokuwa nyuma (wakaangamizwa).

فَأَنجَيْنَاهُ وَأَهْلَهُ إِلَّا امْرَأَتَهُ كَانَتْ مِنَ الْغَابِرِينَ ﴿٨٣﴾

84. Na tukawamiminia mvua kubwa (ya adhabu). Basi tazama jinsi ulivyokuwa mwisho wa waovu (hao).

وَأَمْطَرْنَا عَلَيْهِم مَّطَرًا ۖ فَانظُرْ كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ
الْمُجْرِمِينَ ﴿٨٤﴾ ع

85. Na kwa watu wa Madyan (tulimpeleka) ndugu yao, Shueb, akasema: "Enyi kaumu yangu! Muabuduni Mwenyezi Mungu, hamna mungu mwengine isipokuwa Yeye. Zimekwisha kukufikieni hoja dhahiri kutoka kwa Mola wenu. Basi kamilisheni sawasawa vipimo (vya vibaba) na mizani (pia) wala msiwapunguzie watu vitu vyao wala msifanye uharibifu katika ardhi baada ya kutengenea kwake. Hivi ndivyo bora kwenu ikiwa nyinyi mumeamini."

وَإِلَىٰ مَدْيَنَ أَخَاهُمْ شُعَيْبًا ۗ قَالَ يَا قَوْمِ
اعْبُدُوا اللَّهَ مَا لَكُم مِّنْ إِلَٰهٍ غَيْرُهُ ۖ قَدْ
جَاءَتْكُم بَيِّنَةٌ مِّن رَّبِّكُمْ ۖ فَأَوْفُوا الْكَيْلَ وَ
الْمِيزَانَ وَلَا تَبْخَسُوا النَّاسَ أَشْيَاءَهُمْ وَلَا تُفْسِدُوا
فِي الْأَرْضِ بَعْدَ إِصْلَاحِهَا ۚ ذَٰلِكُمْ خَيْرٌ لَّكُمْ إِن
كُنتُم مُّؤْمِنِينَ ﴿٨٥﴾

86. "Wala msikae katika kila njia kuogopesha (watu) na kuwazuilia na dini ya Mwenyezi Mungu (wale) wenye kuamini, na kutaka kuipotosha (kuitangazia kwa watu kuwa huo ni upotofu). Na kumbukeni mlipokuwa wachache, naye akakufanyeni kuwa wengi (sasa). Na tazameni jinsi ulivyokuwa mwisho wa waharibifu."

وَلَا تَقْعُدُوا بِكُلِّ صِرَاطٍ تُوعِدُونَ وَتَصُدُّونَ
عَن سَبِيلِ اللَّهِ مَنْ آمَنَ بِهِ وَتَبْغُونَهَا
عِوَجًا ۚ وَاذْكُرُوا إِذْ كُنتُمْ قَلِيلًا
فَكَثَّرَكُمْ ۖ وَانظُرُوا كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ
الْمُفْسِدِينَ ﴿٨٦﴾

87. "Na kama liko taifa miongoni mwenu lililoamini yale niliyotumwa kwayo, na taifa (jingine) halikuamini, basi subirini mpaka Mwenyezi Mungu ahukumu baina yetu. Naye ndiye Mbora wa wenye kuhukumu."

وَإِن كَانَ طَائِفَةٌ مِّنكُمْ آمَنُوا بِالَّذِي أُرْسِلْتُ بِهِ
وَطَائِفَةٌ لَّمْ يُؤْمِنُوا فَاصْبِرُوا حَتَّىٰ يَحْكُمَ اللَّهُ
بَيْنَنَا ۚ وَهُوَ خَيْرُ الْحَاكِمِينَ ﴿٨٧﴾

---

wakikaa Falastin (Palestine) na miji iliyokuwa karibu na hapo. Watu hao walikuwa wamcharibika kweli kweli katika akhlaki (tabia) zao.

Hao ndio watu wa mwanzo kuzua machafu ya wanaume kuwaingilia wanaume wenzao. Wakawa hawana haja ya wanawake kabisa.

Basi Mwenyezi Mungu akawapelekea Nabii Luti—ambaye ni mtoto wa ami yake Nabii Ibrahimu na mfuasi wake Nabii Ibrahimu wa mwanzo. Alikuwa mfuasi wake tangu Nabii Ibrahimu alipokuwa Iraqi hata akenda Misri hata akaja Shamu. Kote alikuwa pamoja naye wakilingania watu kheri.

Na katika maasi yaliyokamatana na tupu hapana yaliyowekewa adhabu kubwa zaidi kuliko haya, kwa taathira yake mbaya.

85. Hao kina Madyan walikuwa ni watu waliokuwa wakikaa pande za pwani ya Shamu. Walikuwa wafanyaji wa biashara wakubwa wa zama hizo. Wakatengenekewa barabara kama tunavyosikia katika Historia hao Phoenicians walivyokuwa.